

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na kuzungumza na washiriki pamoja viongozi mbalimbali wanaohudhuria Mkutano wa Jukwaa la Uchumi Duniani, jijini Davos, nchini Uswizi jana. **PICHA: IKULU**

# Timu kuchunguza matukio ulawiti shuleni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeunda timu kuchunguza vitendo vya ukatili wa kingono na udhalilishaji wanavyofanyiwa wanafunzi katika baadhi ya shule nchini.

Hatua hiyo ya serikali imekuja siku moja baada ya gazeti hili kuchapisha ripoti maalumu inayofichua vitendo hivyo dhidi ya wanafunzi katika baadhi ya shule za bweni na kutwa.

Timu hiyo inajumuisha Kamishna wa Elimu, Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora wa Elimu na Mwanasheria wa Wizara ya Elimu ambao watachunguza na baadaye kutoa ripoti ili hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya vitendo hivyo.

Vile vile, serikali imesema Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, leo atatambulisha kwa umma namba maalumu ambayo itaanza kutumika kutoa taarifa za vitendo vya ulawiti katika maeneo mbalimbali ili hatua stahiki zichukuliwe.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akitoa kauli ya wizara kuhusu taarifa za watoto kufundishwa vitendo hivyo vichafu shuleni. "Tupo hapa pamoja na Naibu Waziri Kipanga na Katibu tunataka kutoa kauli kuhusu taarifa ambazo zilitoka kwenye baadhi ya vyombo vya habari kuhusu shule ambazo watoto wamekuwa wakifundishwa tabia mbaya za kulawitiana, tumezichukua kwa umuhimu mkubwa sana.

"Tumeshtushwa sana na taarifa hizo, tumeamua kumpeleka Kamishna wa Elimu mwenyewe sio mwakilishi wake, Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora wa Elimu mwenyewe sio mwakilishi wake pamoja na mwanasheria wa wizara waende haraka sasa hivi wanapitia hizo shule zilizotajwa kujaribu kupata 'fact' ukweli wote," alisema Prof. Mkenda.

Pia alisema wamemwomba Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, kusaidiana na timu hiyo ili katika maeneo ambayo yanahusisha masuala ya jinai polisi wachukue hatua mara moja.

"Tunatarajia hawa walioenda watatuletea taarifa kamili na sisi tupo tayari kuchukua hatua stahiki kudhibiti mambo hayo.

"Zaidi ya hayo kwasababu suala hili limetokea katika eneo moja tunajua kunaweza kukawa na taarifa katika maeneo mengine Katibu Mkuu atatangaza kesho (leo) namba ambayo mtu yeyote akijua kuwa kuna kitu kama hicho katika shule yoyote nchini, shule ya umma ama binafsi au chuo chochote anaweza akapiga simu na kutupa taarifa na sisi tutafuatilia," alisisitiza Prof. Mkenda.

Alisema hivi sasa wanaongeza udhibiti nchi nzima kwa kufuatilia matukio hayo kwasababu yanaweza yakachafua taswira ya sekta ya elimu nchini na kuharibu vijana hali ambayo itawafanya wazazi kukosa imani na shule.

"Mtu yeyote anaweza akipiga simu akasema naomba jina langu lisitajwe na kutoa taarifa kwa wizara na sisi kufanya uchunguzi na kudhibiti jambo hilo na wenzetu wa TAMISEMI wanafanya hivyo hivyo," alisema.

Waziri Nkenda alisema, hivi karibu walifanya kikao chini ya uenyekiti wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, kikiwa na lengo la kuandaa mkakati wa kitaifa wa kudhibiti mambo hayo ambayo yamekuwa wakitokea shuleni, nyumbani na njiani.

"Suala hili ni mtambuka sio la wizara moja ndiyo maana katika kikao kile chini ya uenyekiti wa mheshimiwa Simbachawene, nilikuwapo mimi, Waziri Dk. Doroth Gwajima pamoja na wenzetu wa TAMISEMI, makatibu wakuu wetu watarudisha taarifa kwetu ili taarifa yao itumike kuwa na mkakati mzuri wa kitaifa," alisema Prof. Mkenda.

Gazeti hili juzi liliandika ripoti maalumu ikielezea namna watoto wamekuwa wanavyofundishwa vitendo vya kulawitiana katika baadhi ya shule wilayani Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Katika taarifa hiyo Nipashe ilimnukuu mmoja wa wazazi akieleza alivyowaandikisha watoto wake katika moja ya shule Manispaa ya Moshi na baada ya mwaka mmoja kubaini mabadiliko hasi ya kitabia hasa kwa mtoto wao wa kiume waliyempeleka kwenye moja ya shule binafsi Moshi Vijijini.

"Baada ya mwaka mmoja nilirejea na kuwachukua wanangu kurudi shule za kutwa. Siku moja wakati ninaendelea na majukumu yangu nilimwona kupitia dirishani mwanangu wa kiume akimfundisha mtoto wa jirani namna ya kufanya vitendo vya ulawiti.

"Nilisononeka na kukaa na mwanangu nikamdadisi kwa nia ya kutaka kujua wapi alikojifunza tabia hiyo. Mwanangu alinieleza kuwa vitendo hivyo walifundishwa na patron wa wanafunzi wa ile shule nilikompeleka kwa mwaka mmoja.

"Alinieleza kuwa walikuwa wanafundishwa vitendo hivyo nyakati za usiku na walipewa onyo wasitoe taarifa kwa wazazi wala walimu huku wakiahidiwa zawadi," alisimulia mzazi huyo.

Mama huyo alisema mwanawe alimweleza kuwa msimamizi huwapatia watoto mafuta maalum ya kufanyia vitendo hivyo na kwamba mafuta hayo yanawaepusha kupata michubuko.

# Mitazamo tofauti Mch. Kimaro likizo miezi miwili, kuhamishwa

**Na Mary Geofrey**

MITAZAMO na maoni kinzani vimeibuka baada ya taarifa kwamba Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Usharika wa Kijitonyama, Dk. Eliona Kimaro, amepewa likizo ya siku 60 na pia kuondolewa katika kituo hicho cha kazi.

Taarifa iliyotolewa na Mchungaji Kimaro mwenyewe juzi usharikani hapo wakati wa semina, ilieleza kuwa amepewa barua ya kwenda likizo ya siku 60 (miezi miwili) na baada ya likizo hiyo, hatarejea tena Kijitonyama bali anatakiwa kuripoti makao makuu ya Dayosisi, Luther House, Dar es Salaam.

Dk. Kimaro alisema aliitwa ofisi ya Msaidizi wa Askofu na Mkuu wa Jimbo la Kaskazini, kufanya nao kikao.

"Nimepewa barua ya likizo ya siku 60, kwa hiyo natumia fursa hii kuwaaga. Kesho (jana) asubuhi atahubiri Mchungaji Anna na ndiye atakuwa mchungaji wenu. Kwa mujibu wa barua, nitarudi Machi 17 lakini sitakuja hapa. Barua inanielekeza kuripoti Makao Makuu ya Dayosisi," alisema.

"Mimi ni Mchungaji wa Lutheran ninakiheshimu kiapo changu cha kichungaji na maadili pia ya kichungaji kwa neema ya Mungu. Kwa maana hiyo, imenilazimu kutii na kwenda kwenye hiyo likizo ya siku 60 na baadaye kuripoti ofisi ya Askofu kama nilivyoelekezwa na ofisi ya Askofu," alimalizia.

Hatua hiyo imeibua hoja zinazokinzana huku taharuki ikitanda miongoni mwa waumini na wafuasi wa KKKT zaidi waliokuwa wakipata huduma, hasa mahubiri yake yaliyokuwa yakiwagusa wengi kutokana na mambo halisi ya kimaisha ambayo amekuwa akiyahubiri.

Jana, majira ya saa 4:00 asubuhi, mikakati ya kupinga uamuzi huo ilianza kusukwa na wafuasi wa mtumishi huyo aliyejizolea sifa ndani na nje ya nchi kutokana na mtindo wake wa kuhubiri neno la Mungu.

Makundi ya Whatsapp na Telegram yalianzishwa yalikuwa na kauli mbiu moja ya 'Bring Back Our Rev. Kimaro', ikimaanisha 'Mrudisheni mchungaji Wetu Kimaro'.

Hadi saa 5:00 asubuhi wafuasi wa kundi la Whatsapp walikuwa wamefika 1,200 wakipanga kuvaa tisheti na kwenda kushinikizwa kurejeshwa kwa mchungaji wao huku wakihamasishana kuvaa fulana zenye ujumbe wa kumrejesha na wengi walikuwa wametoa hadi saizi ya fulana ya kuvaa.

Aidha, jana kuanzia kuanzia saa 11:00 jioni, baadhi ya washarika walianza kukusanyika kwenye viwanja vya kanisa wakiwa na mabango yenye ujumbe mbalimbali na kuanzia kuimba "Tufani inapovuma sana moyoni mwangu..."

### WANACHOLALAMIKIA

Baadhi ya wafuasi na waumini walieleza kwenye ujumbe kupitia mitandao ya kijamii kuwa walilalamikia kitendo cha uongozi wa Dayosisi kushindwa kusubiri amalize semina aliyoianza ndipo aende likizo.

"Hii ndio 'mistake' (kosa) kubwa iliyofanyika. Ingefanyika (wangemwondoa) baada ya semina kumalizika kidogo, lisingekuwa jambo zito kama ilivyo sasa. Ni kweli walishindwa kusubiri amalize semina? Je, semina itaendelea? Hata ikiendelea kutakuwa na concentration (usikivu) kweli?" Alihoji mmoja wa waumini hao huku akihoji likizo ya wachungaji ni miezi mingapi?

Naye Aisia Marwa alisema kuwapo kwa taarifa za ghafla ndicho chanjo cha kuleta mshtuko kwa wafuasi kutaka kufahamu undani.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti waumini wa kanisa hilo, walisema utaratibu uliotumika wa kumwondoa ni wa 'kihuni' na siyo wa watu wa imani ya Kikristo.

"Hali hii ni kuondoa sintofahamu kwa waumini na kurudisha nyuma imani zao. Hili lililotokea linahitaji ufafanuzi wa kina kutoka Kwa viongozi wa juu wa KKKT Dayosisi ya Mashariki na Pwani. Sababu ni zipi za kusimamishwa miezi miwili?" Alisema Janeth James.

### WATU MASHUHURI WANENA

Naye Askofu wa KKKT Dayosisi ya Karagwe, Dk. Benson Bagonza, aliandika, 'Somo la Kemia Kanisani' kwa kuandika kwa msamiati kuwa 'wivu + tamaa × ujinga wa mamlaka = burudani mitandaoni.'

Kiongozi huyo wa kanisa anayetambulika kwa kuchambua mijadala ya kitaifa nchini kwa mtindo wa misamiati, alisema 'kuna watu wamepigwa na kuumizwa, wasizuiwe kulia.' Pia alisema watu ambao hawajui chanzo, wasizuiwe kuhoji, kuna wanaojua ukweli wote, mitandao si mahali pa kuusemea.

"...Kuna watu wanashangilia. Ni sawa na ngedere wachanga wachekao msitu unaoteketea wasijue jioni watalala wapi. Shoka lipo shinani, Tunaona nini? Mti mbichi? Mkavu utakuwaje? Mchungaji apigwaye ili kutawanya kondoo? Ng'ombe aliyevunjwa mguu ili arejee zizini? Mfalme katili anayefukuza giza kwa kuzima mshumaa? Mtoto mkaidi asiyefaidi mpaka siku ya Idd au Baba mjinga anayekerwa na nyota ya jirani kuliko giza la nyumbani kwake?"

Alimalizia kwa kusema: "Kuna kitu hakiko sawa mahali, tunahubiria wengine maridhiano, sasa turidhiane sisi."

Naye Mbunge wa zamani wa Arusha Mjini (CHADEMA), Godless Lema, kupitia ukurasa wake wa Twitter aliweka video fupi ya Mchungaji Kimaro wakati akitoa tangazo la kuaga kanisa na kuhoji: "Kuna nini kinaendelea?"

Naye aliyekuwa Meya wa Ubungo, Boniface Jacob, kupitia ukurasa wake wa Twitter, alionyesha kusikitishwa na taarifa hizo na kusema: "Poleni sana waumini wote wa KKKT Kijitonyama, Mchungaji Eliona Kimaro hakuwa mchungaji wa Kijitonyama peke yake. Wapiganaji wa madhehebu mengine tulibarikiwa sana na mahuburi yake. Natarajia kumwona Kimaro madhabahuni tena, popote pale. Mizengwe makanisani inatuvuruga sisi wenye imani changa."

# Bashe aagiza kampuni ununuzi wa parachichi kufutiwa kibali

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, ameagiza kufungiwa kibali Kampuni ya Kandia Fresh kutojihusisha na ununuzi na uuzaji wa parachichi ndani na nje kutokana na kampuni hiyo kununua matunda ambayo hayajakomaa kisha kutupa dampo.

Bashe alitoa agizo jana baada ya kusambaa video iliyoonyesha rundo la parachichi zikiwa zimetupwa mjini hapo.

Alisema uaminifu juu ya parachichi ya Tanzania katika masoko ya nje unazidi kushuka, hivyo kama wataruhusu utamaduni wa watu kuchuma parachichi ambazo hazijakomaa, soko lake litaendelea kushuka.

Bashe alisema ni marufuku kuchuma parachichi ambazo hazijakomaa kwa sababu hakuna soko isipokuwa zinakwenda kuharibu soko la kimataifa.

"Hiyo kampuni kama ipo ndani ya mkoa wetu muifute. Kama mliwapa kibali futa kibali chao sawa mkurugenzi? Kama mtataka maagizo kutoka kwangu kwa barua mtaletewa," alisema Bashe. Aidha, alisema wizara imeandaa mwongozo utakaotumika kitaifa kusimamia mnyororo mzima wa uzalishaji wa zao la parachichi.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kisa Kasongwa, alisema tani 11.5 za parachichi zilikamatwa kwa mnunuzi huyo ambazo zilionekana hazifai kusafirishwa na halmashauri ikailipisha faini ya Sh. 300,000 kwa kununua parachichi bila kibali na kutolipa ushuru.

Mkurugenzi Msaidizi wa Maendeleo ya Mazao Wizara ya Kilimo, Samsom Mponela, alisema si mara ya kwanza kampuni hiyo kukutwa na changamoto katika ununuzi wa matunda ya parachichi.

Waziri Bashe alifanya ziara ya kukagua upatikanaji wa mbolea katika maghala mjini hapo. Akiwa katika ghara la Mtewele alielezwa changamoto na Mkurugenzi Mtendaji Mtewele General Traders, Philemon Mtewele, ambaye alimwomba Waziri kuharakisha malipo ya ruzuku ya mwaka 2015/16.

"Tuna hasara ya mtaji lakini mtaji huu umerudi, umekua mdogo baada ya kazi ya aina hii tuliyoifanya mwaka 2015 na 2016. Malipo hayo mpaka sasa hivi hatujalipwa hata shilingi moja," alisema Mtewele.

# Serikali yamaliza mgogoro wa ardhi uliodumu kwa miaka 15

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imemaliza mgogoro wa matumizi ya ardhi Mbarali mkoani Mbeya, uliodumu kwa zaidi ya miaka 15 uliohusisha wakazi wa Bonde la Usangu na Hifadhi ya Taifa Ruaha.

Akizungumza katika kikao cha wadau waliowekeza katika Bonde la Usangu ambao ni wakulima wa mashamba ya mpunga, mashine za kukoboa na wafugaji, alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia eneo la hekta 74,000 kutolewa kwa wakulima na wafugaji.

Majaliwa alisema serikali imefanya maboresho kwenye Tangazo la Serikali namba 28 ambalo litawawezesha wananchi kufanya shughuli za kilimo na ufugaji endelevu kwa kuwezesha baadhi ya vitongoji vilivyotangazwa awali kuwapo ndani ya hifadhi kuachwa nje ya mpaka.

"Hii GN 28 serikali tumeamua kuitafutia ufumbuzi baada ya vikao vingi na wadau kwa faraja kabisa nataka niwaambie tumefikia hatua nzuri itakayoowezesha kila anayejishughulisha na kilimo kuendelea na kilimo chake na kila anayejishughulisha na mifugo kuendelea na ufugaji wake," alifafanua.

Alisema serikali inawahakikishia wananchi wa Mbarali inaendesha shughuli za kilimo kitaalamu na kwa tija.

"Tumeona maendeleo makubwa na ujenzi wa viwanda vya mtu mmoja mmoja na vikundi, serikali inataka kuona shughuli hizo zinakuwa endelevu, tunataka mpanue viwanda vyenu na mzalishe zaidi," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu alisema serikali iliamua kuitoa nje ya hifadhi ranchi ya Usangu kwa ajili ya shughuli za ufugaji wa kisasa.

"GN namba 28 iliingiza ranchi ndani ya hifadhi, lakini ili wafugaji wawe huru tumeindoa na hivyo itakuwa nje, tumeacha na mito kadhaa ambayo itahifadhiwa kwa sheria za mazingira," alisema.

Kadhalika, Majaliwa aliwataka wafugaji kujiamini kwani mifugo ni uchumi.

"Tunataka tuondokane na uchungaji na kuwafanya Watanzania wafugaji kuacha kutembea umbali mrefu na ng'ombe kwani inaondoa thamani ya nyama, tunataka mfuge kisasa," alisisitiza.

Awali, Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alisema maeneo yaliyoondolewa katika hifadhi watahakikisha mpango bora wa matumizi ya ardhi unawekwa ili wananchi waweze kufanya kile ambacho kimepangwa kufanyika kwa wakati huo.

Aliwahakikishia wananchi hao wanapata hati miliki za maeneo yao ili kuzitumia katika shughuli mbalimbali za maendeleo na mpango wa uandaaji utafanyika kwenye vijiji vyote vinavyohusika.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, alisema kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji watumiaji wote wanapaswa kuheshimu sheria ya mazingira.

Naye Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, aliwataka watumiaji wa eneo lililotolewa kwa ajili ya shughuli za ufugaji na kilimo waendelee kulilinda eneo lilobaki.

"Tusifuge wala kulima katika eneo lililobaki eneo hili ni chanzo kikubwa cha maji na sehemu ya utalii," alisema.

Naye Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema ranchi ya Usangu ni kwa ajili ya shughuli za ufugaji tu na isitokee yeyote akafanya tofauti na lengo.

"Tulioko kwenye ranchi tufuge, wengine mnabadilisha matumizi wengine hamfugi lakini mnakodisha watu wanakuja kulima kwenye vitalu, wale mnaolima badala ya kufuga tutawanyang'anya vitalu," alisema Ndaki.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA HUDUMA YA OFISI ZA KUKODI**

**KUMB : ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0109**

MKANDARASI wa Uhandisi, Ununuzi na Ujenzi wa Gati na Kituo cha Upakiaji wa Mafuta katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) katika Ghuba ya Tanga, anakaribisha Makampuni kueleza nia yao kwa:

**Utoaji wa Nafasi ya Ofisi Za Kukodi**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta yasiyosafishwa yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufuo wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa kilomita 2 kutoka ufukweni katika eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA HUDUMA:**
Timu ya Mradi wa BBN inahitaji nafasi ya ofisi kwa ajili ya kukodisha katika JIJI LA TANGA , ziwe na sifa zifuatazo:

- 500m2 ya Nafasi ya ofisi kwa miaka 2 / miezi 24
- Majengo yaliyosafishwa, safi na yaliyofukizwa dawa ya kuua wadudu kitaalamu
- Inapaswa kuwa katika mji wa Tanga na kufikika kwa urahisi
- Nafasi ya Maegesho ya magari & Jenereta ya kwa umeme wa dharura
- Huduma ya Umeme na maji
- Ziwe pekee kwenye jengo/ eneo au ziwe za kuchangia na wengine kwenye uzio.

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**
Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha:

- Hati miliki au Hati Rasmi zinazothibitisha umiliki wa mali na azimio la kukodisha mali hiyo kutoka kwa mmiliki,
- Hati rasmi ikiwa ni pamoja na leseni ya biashara, nyaraka husika na Hati ya Makubaliano au ridhaa ya mmiliki wa mali hiyo
- Michoro ya kimpango au ya usanifu inayoonyesha mpango wa ofisi / jengo ili BBN iweze kutathmini mahitaji,
- Picha za jengo au eneo zilipo ofisi kwa ajili ya BBN kutathmini pamoja na eneo, ikiwa kuna uhitaji wa kufanya ziara
- Pendekezo la viwango au kodi kwa mwezi ikiwa ni pamoja na vigezo na masharti ya huduma zilizopo/ masharti ya kukodisha,
- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha (Ripoti ya ukaguzi wa fedha ya 2021-2022) na rasilimali za kutosha na zinazofaa,
- Kwa kampuni, kufuata kanuni za petroli (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu kwa usemi huu wa maslahi unapendekezwa sana.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa **procurement@bbnjv.com** . **(Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya tarehe **02 Februari 2023 1800hrs** Saa za Tanzania.

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini zaidi yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka:** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

17232302

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA HUDUMA (3rd Party Services) ZA UCHOMELEAJI, UPAKAJI NA NDT**

**ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0017 / ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0018**

BESIX Ballast Nedam Limited, inayotekeleza Huduma za Awali za mradi wa Gati na Kituo cha Upakiaji katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa:

**- Ukaguzi wa kuchomelea chuma, Upakaji na NDT, Ukaguzi wa Utaratibu wa kuchomelea, Uhitimu wa Welder, Mafunzo na Udhibitishaji wa Wakaguzi wa Mradi na vifaa vya kufanyia Destructive Testing.**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha. Gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwa Meli za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**

* Mkaguzi wa kuchomelea (1) - Kiwango cha chini cha CSWIP daraja la 1 au cheti sawa
* Mkaguzi wa Mipako (1) - Kiwango cha chini BGAS/CSWIP Daraja la II, NACE daraja la II, SSPC na ICORR daraja la II
* Mkaguzi wa NDT (1) – Daraja la II (UT, RT, MT, PT) kulingana na ISO EN 9712
* Sifa za Mchomeleaji (Welder) kulingana na EN 9606-1 na ASME BPVC Sehemu ya IX
* Sifa za Utaratibu wa Kuchomelea kulingana na EN 1090 na ASME B31.3
* Mafunzo na uidhinishaji wa wafanyikazi wa mkandarasi wakati wowote inapohitajika kwa uchomeleaji, upakaji rangi maalumu kwenye chuma na NDT.
* Upimaji wa Vifaa vya Mradi kulingana na viwango vya Mradi.

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**
Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuambatanisha:

- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali za kutosha na zenye uwezo kusimamia kandarasi.
- Orodha ya tajriba iliyo na historia ya ugavi ya kazi husika / rekodi inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika utekelezaji wa huduma zinazofanana za huduma za uchomeleaji na mipako kulingana na viwango vya kimataifa vinavyojulikana katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linalolinganishwa.
- Orodha ya kina ya wakaguzi waliohitimu na kuithinishwa,
- Orodha ya vifaa vya NDT na mipako,
- CV za Wakaguzi,
- Sera ya Ubora wa Kampuni na mipango ya Afya, Mazingira na Usalama Eneo la Kazi na uthibitisho: ISO 9001:2015, ISO 14001:2015
- Rasimu/Sampuli ya ripoti ya ripoti katika umbizo la pdf,
- Kuzingatia kanuni za mafuta ya petroli (Local Content) ya 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania,
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu kwa usemi huu wa maslahi unapendekezwa sana.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma, yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu barua pepe kwa **procurement@bbnltd.co.tz (Ukubwa wa Barua pepe na viambatanishi: 20 MBs & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya tarehe **02 Januari 2023, 12:00 jioni** Saa za Tanzania,

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini zaidi yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

17232302

# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kuua mke kwa kumchoma kisu

**Na Kulwa Mzee**

MKAZI wa Vingunguti Majengo, Dibron Saidi, anayedai alimchoma kisu mkewe akafa baada ya kumfumania na mwanamume mwingine akifanya mapenzi kichochoroni, ametiwa hatiani na kuhukumiwa kunyongwa hadi kufa.

Alidai mkewe alimtamkia maneno ya kuudhi kwamba ikiwa hamtoshelezi ataachaje kuwafuata wengine na kwamba maneno hayo yalimpandisha hasira akafanya tukio hilo.

Saidi alitiwa hatiani jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Avodia Kyaruzi, baada ya pande zote mbili kufunga ushahidi.

Hakimu Kyaruzi alisema mshtakiwa alishtakiwa kwa kumuua mkewe kwa kukusudia na kwamba Machi 11, 2018 saa 6:00 usiku, maeneo ya Vingunguti Majengo, alimuua Harriet Justine kwa kumchoma kisu mara tatu.

Alisema upande wa Jamhuri ulikuwa na mashahidi sita na miongoni mwao alikuwapo mjomba wa marehemu ambaye alidai alisikia sauti ikimwita mjomba mjomba na alipotoka nje, alimkuta mshtakiwa akimchoma kisu mkewe.

Katika utetezi wake, mshtakiwa alidai alikuwa akitokea kazini saa 6:00 usiku na kabla hajafika nyumbani, alimkuta mkewe kichochoroni akifanya mapenzi na mwanamume mwingine.

Mshtakiwa alidai alijitahidi kuvumilia maumivu hadi walipofika nyumbani na akiwa, alimhoji mkewe kuhusu tukio hilo lakini alimjibu kwamba yeye hamtoshelezi, hivyo hawezi kuacha kutafuta wanaume wengine.

"Maneno hayo anadai yalikuwa ya kuudhi akashindwa kuvumilia ndipo alipomchoma kisu. Mahakama baada ya kusikiliza ushahidi ina maswali yanayotakiwa kujibiwa. Mahakama inajiuliza je, ushahidi unajitosheleza kumtia hatiani mshtakiwa. Je, mauaji yalikuwa ya kukusudia au la? Na je, mtuhumiwa ndiye aliyeua au hapana?

"Jukumu la kuthibitisha mashtaka ni la upande wa Jamhuri, wanapaswa kuthibitisha kama kifo kilisababishwa na mshtakiwa," alisema.

Hakimu Kyaruzi alisema shahidi wa tatu alishuhudia tukio na ripoti ya daktari ilieleza kuwa kifo cha marehemu kilisababishwa na kuvuja damu nyingi na mwili wake ulikutwa na majeraha matatu.

Alisema mtuhumiwa alidai kweli alimchoma kisu baada ya kutamkiwa maneno ya kuudhi.

"Mahakama inaona maelezo ya mtuhumiwa hayana ukweli. Angeweza kuzuia hasira yake alipomkuta kichochoroni anafanya mapenzi. Kwa nini alishindwa kuzuia hasira hizo alipotamkiwa maneno ya kuudhi?

"Ushahidi wa upande wa Jamhuri unajitosheleza. Mtuhumiwa anatiwa hatiani kwa kosa la mauaji ya kukusudia," alisema Hakimu. Wakili wa Serikali, Tumaini Mafuru, alipopewa nafasi aliiomba mahakama impe adhabu mshtakiwa kwa mujibu wa sheria kwa sababu maisha ya mwanadamu ni zawadi aliyopewa na Mungu mara moja na ikiondoka haiwezi kurudi.

Alidai marehemu alikuwa na watoto watatu na mama yake waliokuwa wakimtegemea na familia imebaki na mateso kwa sababu ya mshtakiwa.

Wakili wa utetezi, Michael Kibindu, aliomba mteja wake apunguziwe adhabu alidai chanzo cha matatizo ni wivu wa mapenzi. Haiwezekani kuwa na wivu kwa mtu usiyempenda, hivyo mteja wake alikuwa na mapenzi mazito kwa mkewe.

"Mteja wangu alipomkuta mkewe na mwanamume mwingine aliongea na mkewe kutaka suluhu lakini mke alikataa na kutoa maneno ya kuudhi yaliyompandisha hasira akafanya tukio lililosababisha kifo.

"Kisu kilichotumika ni nyenzo zake za kazi hakwenda kununua, mteja wangu ni kijana mdogo, ana watoto watatu hawana malezi sahihi, ni mgonjwa hivyo naomba apewe adhabu nafuu," alidai Kibindu.

Baada ya kusikiza shufaa hizo, Mahakama ilimpa adhabu mtuhumiwa kwa mujibu wa sheria, iliamuru anyongwe hadi kufa.

Mahakama ilisema mtuhumiwa anayo haki ya kukata rufani kama hakubaliani na hukumu hiyo.

# TRA yakumbusha nyumba za wageni tozo ya kitanda

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imewakumbusha wamiliki wa nyumba za kulala wageni na hoteli kulipa tozo ya kitanda ambayo ni asilimia moja kwa kila kitanda kilichotumika.

Imesema ni vyema kila mmiliki wa hoteli au nyumba ya wageni akaweka kumbukumbu zake sawa na kuipa serikali kodi hiyo ambayo ni stahiki yake badala ya kusubiri kufanyika kwa ukaguzi.

Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na kituo kimoja cha televisheni kufafanua kuhusu masuala mbalimbali ya kodi.

Alisema tozo hiyo si mpya kama baadhi ya watu wanavyodhani kwa kuwa ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Utalii ya mwaka 2008 na mwaka 2013 ilitungiwa kanuni namna itakavyokusanywa.

Baada ya hapo, alisema TRA ilipewa jukumu la kukusanya tozo hiyo kutokana na Wizara ya Utalii na Maliasili kutokuwa na miundombinu ya kutosha kuikusanya wakati mamlaka hiyo ina ofisi nchi nzima.

"Ilionekana sisi ndio wenye uwezo wa kuikusanya kwa hiyo tukapewa kazi ya kuikusanya na wizara inayohusika na utalii ilipewa kazi moja ya kuleta orodha ya hoteli na nyumba za kulala wageni ya kila Mkoa na Wilaya kwa nchi nzima," alisema Kayombo.

Aidha, alisema orodha hiyo imekuwa ikihuishwa mara kwa mara kwasababu kuna nyumba za kulala wageni na hoteli zinazooongezeka na kuongeza kuwa mpaka sasa orodha waliyonayo ni ya mwaka 2021.

"TRA inachofanya ni kuelimisha wadau hao mara kwa mara kuhusu sheria inayowataka kulipa tozo hiyo na kwamba tozo inayotakiwa ni kwa kila kitanda ambacho kimetumika. Si kwamba tunahesabu vitanda vyote ulipie hapana, ni kile kitanda kilichotumika siku hiyo," alisema Kayombo.

"Watu wasidhani kwamba TRA inakuhesabia vitanda vyote ulivyo navyo na kutaka uvilipe hapana, tunatoza kile tu ulichopata kutoka kwa mteja kwa mfano umepokea Sh. 50,000 ya chumba kutoka kwa mteja aliyelala hapo sisi unatupa asilimia moja tu ambayo ni Sh. 500," alisema.

Aliwataka wamiliki hao kuwa na utaratibu mzuri wa kutunza kumbukumbu na kuwa na mashine ya kielektroniki ya kutoa risiti (EFD) ili kuepukana na udanganyifu unaoweza kufanywa na wahudumu kuhusu idadi ya wateja waliolala siku hiyo.

"Usipokuwa na utaratibu mzuri wa kutunza kumbukumbu unaweza kuibiwa na wahudumu wako, mfano watu wamelala 20 ukaambiwa wamelala watano sasa kama umedanganywa hivyo na wewe utaidanganya serikali," alisema.

Kayombo alisema kumekuwa na mjadala kwamba kwanini watu wanaolala kwenye nyumba hizo hawaambiwi kuhusu utaratibu huo wakidhani kwamba wateja ndio wanalipa tozo hiyo.

"Nimeona huo mjadala na kuna watu wengi walidhani kwamba mtu anayelala kwenye hoteli au nyumba ya kulala wageni ndiye anayetozwa hiyo tozo, haiko hivyo kwasababu anayetozwa ni mmiliki siyo mgeni kama wanavyodhani," alifafanua Kayombo.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA HUDUMA ZA MALAZI / NYUMBA ZA KUPANGA**

**KUMB : ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0030**

MKANDARASI wa Uhandisi , Ununuzi na Ujenzi wa Gati na Kituo cha Kupakiaji Mafuta katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) katika Ghuba ya Tanga, anakaribisha Makampuni kueleza nia yao kwa:

**Utoaji wa Huduma za Malazi**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta yasiyosafishwa yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufuo wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa kilomita 2 kutoka ufukweni kutoka eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA HUDUMA:**
Timu ya Mradi wa BBN inahitaji huduma ya nyumba za kupanga katika JIJI LA TANGA na zenye sifa zifuatazo:
- Nyumba zilizo na samani zote pamoja huduma zote zinazohitajika
- Nyumba ya Chumba 1 cha kulala, vyumba 2 vya kulala vyote vinajitegemea, ziwe nyumba za kujitegemea au kuchangia kwenye uzio mmoja,
- Nyumba ya Kawaida ya Familia yenye vyumba 3 vya kulala au vyumba 4 ziwe za kujitegemea au kwenye uzio wa kuchangia,
- Majengo yaliyosafishwa, safi na yaliyofukizwa dawa za wadudu kitaalamu
- Inapaswa ziwe Tanga mjini na kufikika kwa urahisi
- Ziwe na eneo la Maegesho & Jenereta kwa ajili ya umeme wa dharura
- Ziwe na huduma ya Umeme na maji

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**
Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha:

- Hati miliki au Hati Rasmi zinazothibitisha umiliki wa mali na azimio la kukodisha mali hiyo,
- Michoro ya usanifu inayoonyesha mpango wa nyumba kwa BBN kutathmini mahitaji,
- Picha za nyumba au nafasi inayopatikana kwa BBN kutathmini pamoja na eneo, ikiwa kuna ziara
- Leseni halali ya biashara na usajili
- Pendekezo la viwango vya kodi kwa mwezi ikiwa pamoja na viwango vya huduma, masharti ya malipo na vigeazo vya kukodisha.
- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha (Ripoti ya ukaguzi wa kifedha ya 2021-2022) na rasilimali za kutosha na zinazofaa.
- Kwa kampuni, kufuata kanuni za petroli (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu kwa usemi huu wa maslahi unapendekezwa sana.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa **procurement@bbnjv.com** . **(Upeo wa Ukubwa wa Barua Pepe: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya tarehe **02 Februari 2023 1800hrs** Saa za Tanzania.

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini zaidi yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka:** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

17232302



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA MAGARI YA KUNUNUA NA KUKODI**

**KUMB : ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0023**

MKANDARASI wa Uhandisi, Ununuzi na Ujenzi wa Gati na Kituo cha Upakiaji wa Mafuta katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), anakaribisha Makampuni kueleza nia yao kwa:

**Utoaji wa Magari ya Kukodisha**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta yasiyosafishwa yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufukwe wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa kilomita 2 kutoka ufukweni kutoka eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA HUDUMA:**

Timu ya Mradi wa BBN inahitaji magari ya kukodi kutumika katika JIJI LA TANGA yenye sifa zifuatayo:
- 7 Na. - 4 x 4 double cabins
- 4 Na. - 4 x 4 Stesheni Wagon SUV
- 1 Na. – Basi dogo la abiria (mini bus)
- 1Na. – basi la abiria (town bus)
- 1 Na. – lori dogo la mizigo
- Kisomo cha odometer kisichozidi 100000km au umri usiozidi ya miaka 5 kutoka mwaka iliyotengenezwa
- Magari yenye bima kubwa
- Itatumika mkoani Tanga
- Hakuna Dereva anayehitajika, yataendeshwa na mtumiaje au dereva wa kampuni
- Ina vifaa vyote muhimu
- Warranti na rekodi za matengezo (service records)

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**
Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa:
- Vibali vya biashara na hati zote ikinyesha uzoefu katika shughuli za kuuza / kukodisha magari.
- Kadi ya usajili inayothibitisha umiliki wa gari
- Bima ya gari inayoonyesha uhalali wa bima kutoka kwa mtoa huduma za bima anayetambulika
- Picha za gari ikiwa ni pamoja na usomaji wa odometer na eneo (zilipo), ikiwa BBN inataka kukagua au kuona magari.
- Pendekezo la bei ya kila mwezi ikiwa ni pamoja na, masharti ya malipo na masharti ya kukodisha,
- Wasifu wa kampuni ulio na uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha (Ripoti ya ukaguzi wa kifedha ya 2021-2022) na rasilimali za kutosha na zinazofaa.
- Kwa kampuni, kufuata kanuni za petroli (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu kwa usemi huu wa maslahi unapendekezwa sana.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa **procurement@bbnjv.com** . **(Upeo wa Ukubwa wa Barua Pepe: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya tarehe **02 Februari 2023 1800hrs** Saa za Tanzania.

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini zaidi yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka:** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

17232302

## HABARI KITAIFA

# Mradi wa maji Chalinze kukamilika mwezi Februari

Na Joseph Mwendapole

WAKAZI 200,000 wa Halmashauri za Chalinze na Handeni na baadhi ya vijiji vya Morogoro, wanatarajiwa kuanza kunufaika na huduma ya majisafi kupitia utekelezaji wa mradi wa Chalinze awamu ya tatu, uliogharimu Sh. bilioni 70.

Akizungumzia maendeleo ya mradi huo jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema mradi umetekelezwa kikamilifu kwa asilimia 96 mpaka sasa na kufikia mwisho wa Februari, utakuwa umekamilika.

Alisema tayari kazi mbalimbali za ujenzi zimekamilika ikiwamo ujenzi wa matangi 18 ya kuhifadhi maji yenye ujazo wa lita 500,000 mpaka milioni mbili, vituo vya kusukuma maji 10 na wameshajenga vituo saba, ujenzi wa mtandao wa kusafirisha maji kwa umbali wa kilomita 1,268 pamoja na ujenzi wa vizimba vya kuchotea maji 351 ambavyo vyote vimekamilika.

"Mpaka sasa utekelezaji umeenda vizuri na kazi kubwa imefanyika ndani ya muda uliopangwa. Kazi iliyobaki kwa sasa ni kufunga pampu kwenye mtambo wa maji Wami. Pampu ambazo zimeshafika hivyo ni kazi ya kufunga tu," alisema.

Luhemeja aliongeza kuwa baada ya kazi kukamilika, mkandarasi atafanya majaribio ya kuruhusu maji kwenye mfumo mwisho wa mwezi wa pili kabla ya kuruhusu uzinduliwe rasmi ili wananchi waanze kupata huduma.

Mradi huu utaongeza upatikanaji wa maji kupitia mtambo wa kuzalisha maji wa Wami kutoka lita 500,000 mpaka lita 900,000 kwa siku.

"Tunaishukuru serikali kwa kuwezesha upatikanaji wa fedha kiasi cha Sh. bilion 70 za kutekeleza mradi huu ambao umefikia hatua za mwisho za ukamilishwaji. Ni wakati sasa wa wananchi kujiandaa kupokea huduma pamoja na kutunza miundombinu ya maji," alisema Luhemeja.

Mradi wa maji Chalinze awamu ya tatu utanufaisha wakazi wa halmashauri yote ya Chalinze, sehemu ya kata zilizoko Tanga, Mkata, Morogoro na Bwawani. Pia kata za Kiwangwa, Msata, Miono, Magomeni, Vigwaza, Tarawanda, Bwirigu, Ubena Zomozi, Mbwewe, Lugoba, Fukayose, Mpera, Msoga Kimange, Mandela, Gwata, Magingu, Mkata, Kwa Sungu, Ngerengere, Kidugalo.

Mhandisi Mshauri wa mradi huo, kutoka kampuni ya ujenzi ya Afcons, Dhaval Soni, alisema kazi kubwa imefanyika kwenye mradi na pampu ya kwanza imekwishafungwa kwenye mtambo wa Wami na kazi inaendelea ili kufunga pampu nyingine kwa lengo la kuongeza uwezo wa uzalishaji maji kwenye chanzo hicho.

"Tunaendelea kukamilisha kazi zilizobaki ikiwamo ujenzi wa vituo vya kusukuma maji, na tunaimani ifikapo mwisho wa mwezi Februari tutakuwa tumekamilisha mradi wote kwa asilimia 100," alisema Soni.

Fatma Nasoro mkazi wa Kihangaiko Msata, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuboresha upatikanaji wa maji kwenye eneo lao, akisema kupitia mradi huo ana imani kubwa ya kupata maji muda wote pasipo usumbufu.

Alisema maji yamekuwa yakikatika katika mara kwa mara kwenye eneo lao, lakini kupitia mradi huu ana imani kubwa kuwa maji yatapatikana vizuri.

# SUMAJKT yaongeza magari 17 kuongeza ufanisi wa kazi

Na Romana Mallya

SHIRIKA la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT), limeendelea kujiimarisha kwa kununua magari 17 yenye thamani ya Sh. bilioni 1.647 kwa matumizi ya kiutawala ili kuongeza ufanisi.

Mkuu wa Tawi la Utawala Makao Makuu ya JKT, Brigedia Jenerali Hassan Mabena katika hotuba yake wakati wa uzinduzi wa magari hayo juzi alisema, yatatumiwa na Makao Makuu ya SUMAJKT, Makao Makuu ya Kampuni ya Ujenzi (SCCL) na Kampuni ya Ulinzi ya SUMAJKT Guard.

Alisema mengine ni kwa ajili ya ofisi ya SUMAJKT Kanda ya Magharibi na SUMAJKT Kanda ya Kusini.

Akizungumza mara baada ya uzinduzi huo, Brigedia Jenerali Mabena alisema shirika litaendelea kununua magari ili kuhakikisha majukumu ya wakurugenzi na watendaji yanarahisishwa.

"Ninawapongeza watendaji wa kampuni ya Ujenzi, SUMAJKT Guard na kampuni ya Usafi, kwa jitihada na ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yenu kwa ufanisi hususani maeneo ya ujenzi, huduma ya ulinzi na usafi katika taasisi za serikali na taasisi binafsi na kuliletea shirika na JKT sifa kubwa," alisema.

Aliwataka watendaji wote kufanya kazi kwa bidii, weledi na ufanisi ili kuendana na kasi ya kufikia malengo ya kuanzishwa kwa JKT.

"Uzinduzi wa magari na pikipiki hizi ukawe chachu kwenu watendaji na kuongeza bidii zaidi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali, hali itakayowezesha kupata faida zaidi na kuongeza vitendea kazi vingine," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT Kanali Petro Ngata alisema kati ya magari hayo, matano ambayo ni aina ya Toyota Hilux Double Cabin 2 ni kwa ajili ya wakurugenzi Makao Makuu ya SUMAJKT, manane ambayo ni Toyota Hilux Double Cabin 2.8 ni kwa ajili ya kampuni ya ulinzi ya SUMAJKT Guard.

Alisema gari moja aina ya Toyota Land Cruiser TX ni kwa ajili ya Mkurugenzi Mwendeshaji wa kampuni ya Ujenzi ya SUMAJKT na Toyota Hilux Double Cabin 2.4 kwa ajili ya Meneja SUMAJKT Ujenzi Kanda ya Kusini.

"Gari Toyota Hilux Double Cabini 2.4 ni kwa matumizi ya Meneja SUMAJKT Kanda ya Magharibi na lingine la aina hiyo litatumiwa na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Usafi SUMAJKT," alisema.

Kanali Ngata aliwataka watakaokabidhiwa wahakikishe wanayatunza na kuyatumia kwa matumizi yanayostahili ili yaweze kuleta tija iliyokusudiwa na kudumu kwa muda mrefu.

Kaimu Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Ulinzi SUMAJKT Guard, Meja Essau Nchimbi alisema wana watendaji 15,222 ambapo kati ya wanaume ni 10,904 na wanawake ni 4,318 na wana magari 49, pikipiki 144, mtambo mmoja na mashine nne.

Alisema wamenunua magari manane aina ya Toyota Hilux Double Cabin 2.8 kwa thamani ya Sh. milioni 687.232, ikiwa ni jitihada za kujijengea uwezo wa kiutendaji ili kuendelea kutoa huduma bora.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Usafi na Unyunyiziaji Dawa za Wadudu SUMAJKT, Kapteni Rosemary Katani akifafanua kuhusu gari aina ya Toyota Hilux Pick Up, alisema lina thamani ya Sh. milioni 103.790 ambalo litatumika kwa shughuli za kiutawala kwa kusaidia kutafuta masoko mapya na kuzungukia miradi.

Alisema kampuni hiyo inatekeleza majukumu yake karibu mikoa yote ya Tanzania Bara na wana jumla ya watendaji 1,368 na wanaendelea kununua vitendea kazi yakiwamo magari, maguta na pikipiki kwa matumizi yao na shirika kwa ujumla.


## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kurudia minada ya hadhara kama ilivyohainishwa kwenye tangazo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MAIN | CHEX ENGINEERING LTD | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NAMBA 110 KITALU '15' NA HATI NAMBA 69065 | CHEDIEL GASPER NSHANA | BUNJU-KINONDONI | 21/01/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA ( MARUDIO) |
| TEMEKE | HAPPYNESS GEORGE MKOPI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PATRICK SAMWEL NGAYIWA | KIJICHI MGENI NANI | 23/01/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | NICE CHANDE MOHAMEDY | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | ROSEMARY DESDELIUS HAULE | KWA AZIZI ALLY | 24/01/2023 SAA 11:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | SASI SELEMANI KITUNDU | NYUMBA | MWAJUMA SELEMANI KITUNDU | GOBA | 25/01/2023 SAA 13:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | BUMERA LOGDE AND CO LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | JOACHIM HERONIMUS MWINGIRA | KIGOGO KATI | 26/01/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | MARYAN GENERAL SUPPLIES | NYUMBA | MARYAN KAPAMA | KIMARA | 27/01/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO |
| TEMEKE | IBRAHIM HARUNA MKALIPA | NYUMBA | IBRAHIM HARUNA MKALIPA | MBAGALA KIBURUGWA | 23/01/2023 SAA 14:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | SALUM KONDO MWINYIMKUU | TANDALE MUHALITANI | KONDO MWINYIMKUU | TANDALE MUHALITANI | 23/01/2023 SAA 14:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | FELIX BIRCKMAS ALOYCE | NYUMBA | KASSIAN ANTONY NINDI | TABATA KISUKULU | 05/02/2023 SAA 12:00MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0715868000/0713237650/0762260787/0719974916
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

17231902

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wizi wa mbolea ya ruzuku nani alaumiwe

**KUSHAMIRI** kwa wizi wa mbolea ya ruzuku kunakohusisha watumishi waliopewa jukumu la kusimamia, kunaibua maswali mengi.

Katika matukio kadhaa yanayoripotiwa kuibwa kwa mbolea ya ruzuku, watuhumiwa wanatajwa kuwa ni wale walioaminiwa kusimamia na kuigawa mbolea hiyo.

Hili ni jambo la kushangaza na ukijiuliza unaweza usipate jibu sahihi kwamba ni kulihujumu taifa ambalo linataka wananchi wake wanufaike na mbole hiyo au ni tamaa ya wachache kunufaisha matumbo yao na kuweka utaifa nyuma.

Ni juzi tu Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ameingilia kati na kuwataka wananchi kuwa walinzi wa mbolea ya ruzuku iliyotolewa na serikali kuhakikisha inatumika kwa malengo yaliyokusudiwa ya kuongeza uzalishaji wa mazao katika msimu wa 2022/2023 yanatimia.

Alipotoa agizo hilo alisema kumekuwa na Watanzania wachache wasiokuwa na nia njema kwa kutorosha mbolea kwenda nchi jirani na kuwaacha wenzao bila kuwa na mbolea ya kutosha, 'jambo hili lazima tulikemee na tulisimamie sote ili kuhakikisha mbolea iliyopo nchini ni kwa ajili ya Watanzania, kila mmoja awe mlinzi kwa mwenzake.'

Utoaji wa ruzuku hiyo ya mbolea unalenga kuongeza uzalishaji wa chakula nchini na Waziri Mkuu akasema ni marufuku kuiuza nje.

Awali mbolea iliuzwa kwa zaidi ya Sh. 100,000, lakini Rais Samia aliridhia kutoa ruzuku Sh. bilioni 150 ili ikashushe bei ya mbolea na sasa inauzwa kwa Sh. 70,000.

Katika wizi huo, Waziri Mkuu alibainisha kuwa mkoani Songwe, tani 2,199 zimekamatwa zikipelekwa nchi jirani. Alisisitiza suala la Watanzania kuwa walinzi kwa sababu hiyo ni pesa yao inatoroshwa na wachache, huku malengo ya serikali ikiwa ni kuhudumia Watanzania kwa usimamizi wa Rais Samia.

Baadhi ya watumishi wanaokamatwa kuhusishwa na wizi wa mbolea hiyo wanakiri kuichukua wakidanganya kuwa wanamashamba ilhali hawana.

Wizi huo unatokana na tamaa kwa kuwa baadhi yao huichukua mbolea hiyo na kwenda kuiuza kwa bei ya juu na kuvuruga lengo lililowekwa na serikali la kuwapunguzia wakulima gharama ya kununua kwa bei kubwa.

Kilimo ni uti wa mgongo kwa sababu bila chakula hakuna mtu atakayekuwa na nguvu ya uzalishaji, iwe kiwandani, ofisini, kwenye biashara na hata kwenye mashamba.

Sekta zote zinategemea kilimo ili mazao yatakayopatikana yatumike kwenye chakula na uzalishaji wa bidhaa nyingine viwandani.

Wanaoiba mbolea hiyo tunaweza kuwaita ni wahujumu uchumi kwa sababu lengo lao ni kufifisha dhamira ya serikali ya kutaka sekta ya kilimo iboreke kwa kuzalisha mazao bora kupitia mbolea watakayotumia.


Kama alivyoagiza Waziri Mkuu, suala la ulinzi wa mbolea ni jukumu la kila Mtanzania ili kudhibiti wizi na nchi iweze kusonga mbele.

Nchi nyingine duniani zimefanikiwa kwa sababu zimeweka mkazo kwenye sekta ya kilimo na kuwa wasambazaji wakubwa wa chakula kwenye nchi nyingine.

Umuhimu wa sekta ya kilimo unaonekana inapotokea nchi kuwa na upungufu wa chakula na serikali kuanza kuhangaika kutafuta msaada kwenye nchi nyingine.

Ni wakati sasa wa kutambua kuwa bila kilimo bora uchumi hauwezi kutengemaa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Vyama vya siasa vijitathmini 2023

**VYAMA** vya siasa vinapoanza kampeni za kuanzisha harakati za kisiasa na mikutano ya hadhara, ni vyema vianze na kufanya tathmini ya ndani kuhusu malengo yao kisiasa kwa mwaka huu ambao ni kama vimepata nuru mpya.

Kwa vyama hivyo, ajenda kuu si kutumia mikutano ya hadhara pekee na kuanza kampeni na hamasa nchi nzima, lakini pia kuwe na suala la miradi ya maendeleo ndani ya taasisi hizo, kuongeza mapato, kutafuta rasilimali zaidi ili kuwa na ofisi, vitendea kazi na kuanzisha mwanzo mpya wa kisiasa kwa kusambaa na kuifikia kila koma ya Tanzania.

Lakini, vyama vijifanyie kujua kama vina kitu gani cha kujivunia licha ya kuwa kifungoni kwa miaka saba. Katika masuala ya kidemokrasia za ndani je, vimefikia malengo? Vimefundisha makada wangapi itikadi au msimamo wao? Je, wametoa au hawakutoa mafunzo ya uongozi?

Kama havikufanya vizuri katika kufikia malengo hayo tatizo ni nini? Je, ufumbuzi uko wapi?

Kwa mfano kuna kufanya tathmini ya majukumu, wameweza kuwa na ofisi au kutenga kiasi fulani cha fedha ili kufikisha Shilingi milioni 100 kununua kiwanja, au kama kuna ardhi kujenga ofisi ili kujipunguzia gharama za kupanga ambazo ni kubwa na zinazorudisha nyuma mipango mingine ya maendeleo?

Pamoja na hayo ni vyema pia kuwa makini kwenye masuala ya matumizi ya pesa za chama, hadi sasa zimetumika kiasi gani? Je, kuna faida katika matumizi hayo? Suala la demokrasia na uenezi ndani ya chama ni muhimu. Vipi kuhusu kufikia malengo ya kushirikisha wanawake na vijana kwenye uongozi.

Uchaguzi mkuu wa 2025 unahitaji maandalizi chama kinajiwekea rasilimali na fedha kiasi gani ili kifanye vizuri ? Ni mambo gani mabaya yanaweza kukikwamisha katika kutekeleza malengo kipindi cha kuelekea mwaka wa uchaguzi.

Wanasiasa wawe na mitizamo chanya ili waweze kujiongezea nafasi za kukubalika waangalie changamoto kama fursa ili 2025 iwe ya shangwe ya maendeleo ya demokrasia hata baada ya kukaa jela kwa karibu muongo mzima.

Ikumbukwe mwaka 2024 ni uchaguzi wa serikali za mitaa ni muda wa kujiongezea kipato, kutumia vipaji walivyo navyo wanasiasa wetu, ili kufanikisha azma ya kuwa vyama mbadala vinavyochangia kubadili sura ya nchi na kuleta maendeleo.

Wanasiasa hawa wanaweza kwenda katika taasisi za elimu ya juu na hata za kitafiti ili kujiongezea uwezo wao, wapate semina na kufuliwa ili waweze kuwa bora zaidi majukwaani kwenye kampeni za uchaguzi wa mitaa na ule mkuu.

Vyama vya siasa vijihusishe na shughuli mbalimbali za kiuchumi kama vile kilimo kwenye maeneo mengi nchini kuna ardhi zenye rutuba, kuzalisha mali si jambo baya ili kuwa na mapato.

Vinapohimiza Tanzania kujitegemea na kupunguza utegemezi kwa nchi za kigeni viwe mfano siyo kuendeleza kanuni ya sikiliza mawazo yangu usiangalie matendo yangu.

Wananchi wanategemea kuwaona wanasiasa wakijitolea na kushiriki kwenye masuala mbalimbali ya maendeleo na raia mitaani mfano, kuchimba na kutengeneza mitaro ya majitaka, kusaidia shughuli za nguvu za wananchi kama kufyatua matofali, kujenga vyoo shuleni na kazi kijamii badala ya kusimama pembeni na kujitenga na wananchi kwa kisingizio kuwa hawako madarakani na kwamba ni jukumu la CCM.

Wakumbuke zama hizi ni za siasa za kijasiriamali kutokana na mazingira kubadilika kuanzia tabianchi, teknolojia na utandawazi hivyo kwa mwanasiasa naye anatakiwa kubadilika pia.

Wanasiasa wawe na imani na kile wanachofanya siyo kumangamanga na kuwa kama watu wasiofahamu itikadi wala malengo yao ili umma uone kuwa wamedhamiria na wanafanya siasa za kuwaomba, kuishauri na kuikosoa serikali ili kuwaondolea Watanzania matatizo ya kiuchumi na umaskini waliyonayo.

HABARI KITAIFA

## Kifo cha mtoto kutumbukia kwenye dimbwi chazua utata

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MWANAFUNZI wa Shule ya Msingi Sunflower Ilula, Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa, Kian Msamba (6), amedaiwa kufa maji kwa kutumbukia kwenye dimbwi lililokuwa ndani ya uzio wa shule hiyo na kifo chake kuzua utata.

Tukio hilo limetokea Januari 14 majira ya mchana wakati wa mvua inayoendelea kunyesha mkoani humo.

Wakizungumza baada ya maziko, wazazi pamoja na ndugu waliomba uchunguzi ufanyike katika shule hiyo kwa kushindwa kusimamia malezi ya watoto wanaokabidhiwa na kuwapo taarifa tata za kifo cha mtoto wao.

"Tunaomba timu iundwe ili kuchunguza tukio hili kwani mpaka sasa uongozi wa shule haujasema lolote wala kutoa historia yoyote ya mtoto katika kipindi chote walichokuwa wanaishi na mtoto wetu," alisema Elisha Kivike, mwananchi wa eneo hilo.

Atilio Mwalisa, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Uyole 'A', alisema taarifa ya kifo waliyopokea haikuwa kamili ndiyo maana hata makaburini walitangaza ni ajali ya maji.

Alitoa rai kwa wamiliki wa shule kuwa makini na watoto hasa kipindi hiki cha mvua.

Baba mzazi wa mtoto huyo, Kornel Msamba, alisema siku ya tukio alipigiwa simu na uongozi wa shule na kutakiwa kufika Hospitali ya Ilula haraka kwa madai kuwa mtoto wake anaumwa, lakini alipofika alikuta polisi ambao walimpa taarifa ya kifo cha mtoto wake.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Dickson Malamala, alisema wakati mtoto anafikishwa hospitali alikuwa ameshafariki na walikamilisha vipimo vingine ili kujua chanzo cha kifo chake.

"Mwili wa mtoto ulikuwa ukitokwa na maji puani na mdomoni na kifo chake kimesababishwa na maji," alisema.

Mkuu wa shule hiyo hakuweza kupatikana kwa kuwa anashikiliwa na Polisi pamoja na Mkurugenzi wa shule hiyo huku Mwalimu Mkuu Msaidizi, akidai sio msemaji, lakini alikiri kuwapo kwa tukio hilo.

"Nashindwa kuzungumzia tukio hili kwani sifahamu chochote zaidi ya kusikia juu ya kifo cha mtoto huyu aliyefia hapa shuleni kwenye dimbwi la maji jirani na geti la kuingia shule," alisema.



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza jana. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Kesi kupinga kuachiwa huru Sabaya kuanza kusikilizwa siku 5 mfululizo

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha, itaanza kusikiliza siku tano mfululizo rufani iliyowasilishwa na Jamhuri kupinga hukumu ya kumwachia huru aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, ya uhujumu uchumi iliyotolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha.

Katika rufani hiyo waleta rufani ni Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), wajibu rufani ni Ole Sabaya na wenzake watano, Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Naibu Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Judith Kamala, alisema rufani hiyo itaanza kusikilizwa Februari 27, 28 na Machi 1, 2 na 3, mwaka huu, chini ya Jaji wa Mahakama hiyo, Salma Maghimbi.

"Rufani hii itaanza kusikilizwa baada ya kutolewa kwa chapisho kwenye magazeti mara tatu ya kuitwa kufika mahakamani kwa warufani ambao waliachiliwa huru," alisema.

Wakili wa Serikali, Alice Mtenga, alidai rufani ilipangwa kwa ajili ya kusikilizwa baada ya kutekelezwa kwa agizo la mahakama kwa kuagiza kutolewa kwa chapisho mara tatu kwenye magazeti la kuitwa kufika mahakamani kwa warufani ambao waliachiwa huru.

Naye Wakili wa mjibu rufani wa kwanza (Sabaya), Mosse Mahuna, alidai hawana pingamizi na hoja ya wakili wa waleta rufani kwa ajili ya kusikilizwa.

Juni 10, 2022, Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, chini ya Hakimu Patricia Kisinda, ilimwachia huru Sabaya na wenzake kwa madai kuwa hati ya mashtaka ilikuwa na upungufu kisheria.

Hakimu Kisinda, alisema mahakama hiyo, ilipitia ushahidi wa pande zote mbili na kuuchambua kwa kina kulingana na mashtaka ya kisheria na ilijiridhisha ushahidi uliotolewa kwa kuwa haukuweza kuthibitisha mashtaka hayo pasipo shaka yoyote.

"Kutokana na sababu hiyo mahakama imewaachia huru washtakiwa wote kwa makosa waliyoshtakiwa mahakamani," alisema Kisinda.

Katika shauri hilo, shtaka la kwanza ni la kuongoza genge la uhalifu kinyume na Sheria ya Uhujumu Uchumi Kifungu cha 57(1) na 60(2) lilikuwa linawakabili washtakiwa wote.

Shtaka la pili, kujihusisha na vitendo vya rushwa na lililokuwa kwa mshtakiwa wa kwanza peke yake na ni kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu cha 15(1B,2) sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Shtaka la tatu, kujihusisha na vitendo vya rushwa, lilimkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake, kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu cha 15(1B,2) sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Shtaka la nne, matumizi mabaya ya madaraka, lilimkabili Sabaya, shtaka la tano, utakatishaji wa fedha na liliwakabili washtakiwa wote.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Baadhi wauguzi watuhumiwa kuuza vifaa vya kujifungulia

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WANANCHI wa Manispaa ya Singida wamewasilisha malalamiko kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, kuhusu baadhi ya wauguzi vituo vya afya na zahanati kikiwamo cha Sokoine kuwauzia vifaa vya kujifungulia.

Waliwasilisha malalamiko hayo jana katika mkutano na mkuu huyo ambaye ameanzisha utaratibu wa kukutana na wananchi kila wilaya kusikiliza kero kwa kuanzia katika Manispaa ya Singida.

Katika kikao hicho, kero ya migogoro ya ardhi ilikuwa 15, malalamiko kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) yalikuwa mawili, uchafu kukithiri kwenye dampo lililoko eneo la Bohari Manispaa ya Singida.

Madai mengine ni wauguzi wa Kituo cha Afya cha Sokoine kulalamikiwa kuwauzia vifaa vya kujifungulia wajawazito wakati vinatolewa bure na serikali, huku kukiwa na madai ya wananchi ya kurudishiwa fedha walizozitoa kwa ajili ya kupatiwa vibanda vya biashara kituo cha mabasi Misuna.

Kutokana na malalamiko hayo, Serukamba aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza malalamiko ya wananchi waliouziwa viwanja ambavyo vina wamiliki zaidi ya mmoja na baadhi ya vituo vya afya na zahanati vinavyolalamikiwa kuuzia wananchi vifaa tiba.

Aliwataka watumishi mkoani humo wanaoshughulikia masuala ya ardhi kufanya kazi kwa weledi na kuwatendea haki wananchi ili kuondoa migogoro ya ardhi ambayo imekuwa kero kubwa kwa wananchi.

Aliwataka watendaji wa Idara ya Ardhi katika Manispaa ya Singida kufuata sheria na kuwatendea haki wananchi ili kuepuka uuzaji wa viwanja ambavyo tayari vinaumiliki wa watu wengine.

"Katika kero zote zilizotolewa na wananchi ni dalili ya kwamba watumishi hatujafanya kazi yetu vizuri, wananchi bado hawajapewa elimu ya kutosha kwa hili tunatakiwa kubadilika," alisema.

Pia aliwataka watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida wajenge tabia ya kuwatembelea wananchi na kujua changamoto walizonazo ili kuzitafutia ufumbuzi na wanapozitatua wafuate sheria na kutenda haki.

Aliagiza manispaa hiyo kuondoa taka zote kwenye makazi ya watu na maeneo mengine na kuomba Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) wanapojenga barabara wasisahau kuweka miundombinu ya mifereji ili kusaidia mji kuwa safi wakati wote.

Baadhi ya wananchi waliotoa kero ya ardhi ni Abdallah Somb na John Natumwa ambaye alidai kutoa Shilingi milioni tatu kwa ajili ya kupatiwa kibanda cha biashara stendi ya mabasi ya Misuna na Mkuu wa mkoa kuagiza manispaa kumrudishia fedha hizo mara moja.

Wengine waliotoa kero zao ni Ishimaeli Rajabu na wenzake wanane wanaoishi eneo la mnada wa zamani wa Karakana ambalo licha ya kuomba wapimiwe kumekuwa na danadana na kuwafanya washindwe kuliendeleza kwa kujenga nyumba.

Kero nyingine iliyotolewa katika kikao hicho ilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Super Kitasa Enterprises, Didas Ngowi, ambaye alisema anaidai Manispaa ya Singida Sh. milioni 77 baada ya kampuni hiyo kupewa zabuni ya kuzoa taka katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2013, 2014 na 2015.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Jeshi Lupembe, alikiri kuwapo kwa deni hilo na mchakato wake upo tayari na kuwa fedha hizo zitalipwa mwaka wa fedha wa 2023/2024.



Mjumbe wa Baraza Kuu UVCCM Taifa, anayewakilisha Mkoa wa Lindi, Ramadhan Matola (mwenye kipaza sauti), akizungumza na vijana wenzake wa Wilaya ya Nachingwea juzi, wakati akiwahimiza kutangaza mema yanayofanywa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa ajili ya maendeleo ya Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanachama CCM watakiwa kujiandaa kujibu hoja

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Pwani, Jackson Kituka, amesema ni jukumu la wanachama kujiandaa kuelezea wananchi kwenye mikutano ya hadhara kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali uliofanywa na serikali.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza kwenye Baraza la Jumuiya hiyo lililofanyika Kibaha kuwa baada ya kuruhusiwa mikutano ya hadhara yapo mambo mengi yatasemwa na vyama vingine na kuwataka kujiandaa kujibu kwa vielelezo.

"Fikeni kwenye ofisi za wakuu wa wilaya mkapate taarifa za miradi iliyotekelezwa na serikali ambayo imetatua kero za wananchi, msinyamaze kimya serikali ikishambuliwa," alisema.

Alisema viongozi waliochaguliwa hivi karibuni wanatakiwa kufanyakazi kwa ushirikiano na kuepuka migogoro itakayosababisha baadhi ya majukumu kutofanyika kwa ufanisi.

"Sitaki kuwa mwenyekiti wa migogoro kaeni mfanye kazi vizuri jiandaeni kujibu yale yatakayokuwa yanasemwa vibaya kwenye mikutano ya hadhara mkiwa na takwimu ya kila eneo nini kimefanyika na fedha zilizotumika mkajibu pale mnapoona kuna upotoshaji," alisema.

Awali, Katibu wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Pwani, Elisante Msuya, alisema wajumbe kutoka katika wilaya za mkoa huo wameshiriki katika baraza hilo la siku mbili lililoambatana na kuchagua wajumbe kamati ya utekelezaji.

Alisema wajumbe wa baraza walipata fursa ya kupatiwa semina ya mazingira, changamoto zake zinazoukabili mkoa wa Pwani, Sera ya Elimu, Sera ya Malezi na changamoto za kimalezi kwa mkoa huo.

Alisema baada ya baraza hilo wajumbe watakwenda kusimamia walioyojifunza kwa kuhakikisha utunzaji mazingira unaimarika pamoja na malezi ya watoto ikiambatana na kuhamasisha jamii ya mkoa huo kujenga tabia ya kuwa karibu na watoto wao kusimamia maadili yao na kuipa elimu kipaumbele.

Selina Koka, alichaguliwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Pwani pamoja na Judith Muluge, Hemed Salim na Dk. Michael Benedict.

# Morogoro yapokea bil. 16/- kuboresha kilimo

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKOA wa Morogoro umepokea Sh. bilioni 16 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya sekta ya kilimo zitakazotumika kuboresha miundombinu ya umwagiliaji na ujenzi wa maghala.

Mkuu wa Mkoa huo, Fatma Mwassa, alisema wakati akielezea mikakati mbalimbali katika uendelezaji na ukuzaji wa sekta hiyo mkoani humo.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 15 zitatumika katika ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji na Shilingi bilioni moja ni kwa upande wa maghala.

"Rais wetu Dk. Samia Suluhu Hassan, tunamshukuru kwa kutupatia fedha hizo kwenye sekta ya kilimo na miradi yote hii iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji," alisema Mwassa.

Alisema Mkoa wa Morogoro unashika nafasi ya nne kwa uzalishaji wa chakula nchini na namba moja katika uzalishaji wa mpunga na miwa na nafasi ya sita katika uzalishaji wa ndizi.

"Lengo letu kama mkoa ni kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, kwani mpunga ndilo zao kuu katika mkoa wetu na Tanzania kwa ujumla mkoa unashika nafasi ya kwanza katika uzalishaji," alisema Mwassa.

Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Morogoro, sehemu ya Uchumi na Uzalishaji, Dk. Rozalia Rwegasira, alisema mkoa huo kwa msimu wa mwaka 2021/2022 ulilenga kuzalisha tani 3,035,485.9 za mazao ya biashara kutoka kwenye hekta 940,509.07.

Alisema, katika msimu huo uzalishaji ulikuwa ni tani 1,775,511.7 sawa na asilimia 58.5 na hekta 681,485.9 zilitumika ni sawa asilimia 72.

Mazao ya biashara katika msimu huo mkoa ulipanga kuzalisha tani 2,704,383.9 katika hekta 205,083.8, lakini uzalishaji ukiwa ni tani 1,743,853 sawa na asilimia 64 kutoka kwenye hekta 155,773.8 ambazo ni sawa na asilimia 76.

Kwa msimu wa 2022/23 mkoa unatarajia kulima mazao ya chakula kwa hekta 936,448 ili kuzalisha tani 3,068,101 na mazao ya biashara tani 2,900,321 kwa hekta 226,900.

Dk. Rwegasira alisema katika msimu wa mwaka 2022/2023 mkoa huo unatarajia kulima mazao ya chakula kwa hekta 936,448 ili kuzalisha tani 3,068,101 ya mazao ya chakula na tani 2,900,321 kwa hekta 226,900 kwa mazao ya biashara.





## Kiama cha wanaochafua vyanzo vya maji chanukia

**Na Oscar Assenga,** MUHEZA

KIAMA dhidi ya wananchi wanaoendelea kufanya shughuli za binadamu kama kilimo, ufugaji na ujenzi wa makazi, karibu na vyanzo vya maji licha ya kuwapo zuio la kufanya hivyo 'kinanukia.'

Jana, Mkurugenzi wa Bonde la Pangani (PWB), Segule Segule, alisema kazi inayoendelea sasa kabla ya kuchukua hatua ni kubaini maeneo yote yaliyovamiwa na yameathiriwa kwa namna gani na shughuli za binadamu.

Segule alitangaza ujio wa kiama hicho alipotembelea na kukagua vyanzo vya maji vinavyotiririsha maji kwenye Mto Zigi. Segule alisema kazi hiyo ni utekelezaji wa agizo la Waziri wa Maji, Jumaa Awesso, alilolitoa wiki iliyopita akiwa jijini Tanga.

"Tutachukua hatua kali za kisheria ili kukomesha vitendo hivi katika vyanzo vya maji. Kwa gharama yoyote tutahakikisha vyanzo vya maji vinaendelea kuwa salama bila kuvamiwa na kuharibiwa kutokana na shughuli za binadamu," alisema.

Segule alisema wamekuwa wakielekeza nguvu zaidi kwenye kutoa elimu, wakiamini kwamba watu wakibadilisha mawazo yao wakielewa na hivyo itakuwa ni rahisi kujisimamia wenyewe, lakini jambo hilo ni tofauti.

Akiwa kwenye chanzo cha maji cha Mto Muze, ambao ni moja ya mito midogo inayomwaga maji yake Mto Zigi, Mkurugenzi huyo, alisema tathmini inaonyesha kuwa maji yanayochafua Mto Zigi ni kutoka Mto Muze, ambao umejaa tope kwa kiasi kikubwa.

Alizitaja pia shughuli za ujenzi zinazoendelea upande wa juu ya Mto Muze, zilizohusisha kutifua ardhi na ujenzi wa madaraja, ndivyo vilivyochafua maji yanayotumiwa na binadamu katika chanzo cha Mabayani kinachotumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Tanga (TANGA-UWASA).

"Lakini bado wapo wakulima wanaolima kandokando ya mto huo na kufanya udongo usiwe imara, matokeo yake udongo unasombwa na kuingia kwenye mto. Halafu pia kunakuwapo na kumeguka kwa pande kubwa la udongo kutokana na kuchochewa na shughuli za binadamu," alisisitiza Segule.

# Spika aweka msimamo sheria za kupambana na ukatili kijinsia

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amesema Bunge liko tayari kurekebisha au kufuta kabisa baadhi ya vipengele vya sharia vinavyowapa faida kisheria wanaofanya makosa ya ukatili wa kijinsia nchini kukwepa adhabu.

Aidha, amesema Bunge litafanya hivyo wakati wowote kuanzia sasa kama serikali itaamua kupeleka Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ili kufumuliwa na kutungwa mpya zinazodhibiti vitendo hivyo.

Dk. Tulia alikuwa akizungumza jana jijini Tanga hapa alipokuwa akifungua Mkutano Mkuu wa 11 wa Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake Tanzania (TAWJA).

"Kutokana na udhaifu wa kisheria unaoonekana katika baadhi ya sheria. Nawasihi TAWJA kuainisha vipengele mnavyoona vinamlinda mtuhumiwa kwa kutoa mwanya wa kuachiwa huru, wakati kosa limefanyika.

"Iombeni serikali ilete marekebisho ya vipengele hivyo bungeni ili viangaliwe na kutungwa upya ili haki ipatikane kwa pande zote. Tumalize haya malalamiko ya wananchi kwa kuwaondolea maswali yasiyojibika," alisema.

Dk. Tulia alisema kwa kawaida wananchi wanapomkamata mhalifu aliyefanya ukatili, humpeleka polisi wakijua atafunguliwa mashtaka na kufikishwa mahakamani na kisha kupewa adhabu. Lakini cha ajabu baadaye hushangaa ameachiwa huru, hivyo kuibua maswali na masononeko kwa walliomkamata.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, akizungumza katika mkutano huo, alisema TAWJA imeanza kufanyia kazi kwa vitendo maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoyatoa mwanzoni mwa mwaka huu.

Prof. Juma alisema TAWJA pamoja na mahakama, kazi kubwa wanayofanya ni utoaji haki na kuelimisha umma kuhusu utoaji wa haki za binadamu, kujenga uwezeshaji miongoni mwa wadau wa haki za binadamu, upatikanaji wa haki kwa makundi yaliyoko katika hali hatarishi, wanawake, watoto na watu wenye ulemavu.

"Sisi mahakama tunajivunia sana uwepo wa hiki Chama cha TAWJA, muhimili wa mahakama unakichukulia kama chombo maalumu ambacho kinaleta taswira na muonekano kwamba, mahakama ni taasisi inayojali usawa wa kijinsia na kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa TAWJA, Jaji Joaquine De- Mello, alisema chama hicho kilianzishwa mwaka 200 kama chama cha kijamii, dhima yake kuu ni kusimamia haki na kuona haki sawa zinatolewa kwa wote, kwa kuzingatia utawala wa sheria na usawa wa kijinsia.




Mkurugenzi wa Taasisi ya Zaina Foundation, Zaituni Njovu, akitoa semina kwa waandishi wa habari wanawake kutoka mkoani Arusha na Kilimanjaro, kuhusu kuwajengea uwezo juu ya matumizi ya mitandao ya kijamii pamoja na kujilinda na ukatili wa kimtandao jijini Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# SAU yatangaza rasmi kuanza mikutano

**Na Anjela Mhando,** MOSHI

CHAMA cha Sauti ya Umma (SAU) kimeanza rasmi mikutano yake ya hadhara mkoani Kilimanjaro huku kikieleza kuwa uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan wa kuondoa zuio la mikutano ya kisiasa, unawapa matumaini mapya wapinzani kuingia katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka ujao, wakiwa na Tume Huru ya Uchaguzi.

Akizungumza jana katika Kata ya Bomambuzi, Manispaa ya Moshi, Mwenyekiti wa SAU mkoani Kilimanjaro, Isaac Kireti, alisema matarajio ya vyama vyote vya siasa hapa nchini kwa sasa, ni kuona uchaguzi huo pamoja na uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani wa mwaka 2025 unasimamiwa na tume hiyo.

"Tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuondoa zuio la mikutano hii lililokuwa limewekwa na mtangulizi wake, hayati Rais Dk. John Magufuli mwaka 2016. Huyu ni muumini wa siasa za kistaarabu, amekubali kukosolewa ili afanye kazi yake kwa uwazi na kulijenga taifa letu katika misingi ya haki.

"Kuviruhusu vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara, ni kuwawezesha wananchi kueleza matatizo yao bila ya kuhofu walioko kwenye madaraka. Sasa ni rasmi kwamba wananchi watasema kile wanachofikiri na wanachotamani serikali yao iwafanyie," alisema.

Alisema matarajio ya SAU na vyama vingine vya upinzani ni kuona ikifika mwaka 2024 kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na mwaka 2025 kwenye uchaguzi mkuu, tume hiyo ndiyo isimamie na si halmashauri kama ambavyo zimekuwa zikifanya.

Katika mkutano huo, Kireti alipongeza serikali kwa kuboresha sekta ya afya kwa kuhakikisha kuwa kila mkoa na wilaya kuna kuwa na zahanati, vituo vya afya na hospitali za rufani za mikoa zimejengwa na kuwawezesha wananchi kupata huduma za matibabu bila usumbufu.

"Yako mafanikio makubwa ambayo yamefanyika kwa kipindi kifupi tangu Rais Samia ashike madaraka ya kuiongoza nchi. Tumeshuhudia ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, miundombinu ya maji, miradi ya barabara na ujenzi wa vyumba vya madarasa," alisema.

Kuhusu sekta ya elimu, SAU imesema serikali imefanikiwa kubeba jukumu lake kwa ufanisi la kujenga vyumba vya madarasa na kuwapunguzia wazazi mzigo wa kuchangishwa fedha za miradi ya ujenzi wa vyoo, madarasa na majengo ya utawala, kwa kuwa ilikuwa likiwaumiza wazazi wengi.



# Mama adaiwa kuwachoma wanawe mikono tuhuma ‘kudokoa’ mboga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SCOLASTICA Peter (28), mkazi wa Ibinzamata Manispaa ya Shinyanga, anadaiwa kuwajeruhi watoto wake wawili kwa kuwachoma moto mikono kwa tuhuma za kuiba mboga.

Mtendaji wa Kata ya Ibinzamata, Victor Kajuna, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake.

Alisema baada ya tukio hilo, mwanamke huyo alikamatwa na wasamaria wema na kupelekwa katika ofisi ya mtendaji pamoja na watoto hao.

Akizungumza na waandishi wa habari, mtendaji huyo alisema juzi saa 4:00 asubuhi, aliwaona wananchi wakienda ofisini kwake na watoto wawili ambao wamechomwa moto mikono yote na alipohoji akaambiwa mama yao ndiye amefanya hivyo na wako naye.

Kajuna alisema baada ya kumhoji mwanamke huyo kuhusu ukatili huo, alikiri kuwa ni kweli amewachoma moto mikono yao kwa madai kuwa wamekuwa na tabia ya kudokoa mboga kila mara.

“Alichokifanya mwanamke huyu kwa watoto hawa ni ukatili mkubwa na sisi kama viongozi tutamchukulia hatua kali za kisheria ili liwe fundisho kwa wazazi wengine,” alisema.

Mwanamke huyo alipohojiwa na vyombo vya habari kuhusu kuwachoma moto mikono watoto wake, alikiri kuwa ni kweli amefanya hivyo ili waache tabia ya kudokoa mboga kila mara.

Alisema watoto amekuwa akiwakanya kila mara kuacha tabia ya kudokoa mboga, lakini hawasikii na siku aliyowachoma moto mikono walikomba dagaa ambao waliwabakiza usiku.

“Hawa watoto wana tabia ya udokozi na siyo mara ya kwanza kuwapatia adhabu, nilishawapiga na nyaya, lakini hawasikii, jana usiku tulibakiza mboga, asubuhi nilipokwenda kwenye mihangaiko yangu narudi nyumbani nakuta wamekomba mboga yote, nikaona niwachome moto mikono ili niwakomeshe kabisa,” alisema Peter.



Watoto wawili wakazi wa Ibinzamata, Manispaa ya Shinyanga, wakiwa katika Ofisi ya Mtendaji wa Kata ya Ibinzamata juzi, wakionyesha majeraha mikononi baada ya kuchomwa moto na mama yao mzazi, Scholastica Peter (hayupo pichani), wakidaiwa kukomba mboga. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Asasi ya wanawake yalaani matukio ya mauaji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

ASASI ya Wanawake Laki Moja ambayo inajihusisha na utetezi wa haki za wanawake na watoto mkoani Shinyanga, imelaani matukio ya mauaji dhidi ya wanawake na watoto yanayoendelea kutokea.

Mwenyekiti wa Asasi hiyo, Anascholastica Ndagiwe, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani Shinyanga kutoa tamko la kulaani kukithiri kwa mauaji dhidi ya wanawake na watoto.

Alisema katika Mkoa wa Shinyanga kuna matukio ya mauaji dhidi ya wanawake ambayo yanatokana na vipigo kutoka kwa waume zao, na kuiomba serikali kupitia vyomba vya dola idhibiti mauaji hayo kwa kushirikiana na viongozi wa seeikali za mitaa.

“Mauaji mengi ya wanawake mkoani Shinyanga yamekuwa yakitokea kwa uzembe wa viongozi na majirani, unakuta mwanamke anapigwa na anaomba msaada, lakini watu hawamsaidii wanabaki kutizama hadi anapoteza maisha,” alisema Ndagiwe.

“Mwanamke akishafariki ndipo wanatokea mashuhuda na kusema tulisikia wakati anapigwa na alikuwa akiomba msaada, tunaomba tabia hiyo ife, badala yake tutoe msaada pale mwanamke anapokuwa akipigwa na kuomba msaada ili kudhibiti mauaji ya wanawake yasiendelee Shinyanga,” aliongeza.

Alitoa mfano kuwa Januari 14, mwaka huu, Joyce Masanja aliuawa kwa kupigwa na kisha kuchomwa kisu na mume wake Thomas Mathias na kabla ya kifo alikuwa akiomba msaada, lakini hakupata hadi akapoteza maisha.

Mwenyekiti wa kikundi kazi cha mashirika yanayotekeleza mradi wa kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto mkoani Shinyanga, Paschali Mbugani, alisema mauaji ya wanawake kuendelea kutokea mkoani humo ni uvinjifu wa haki za binadamu.

Alitoa wito kwa wanandoa wanapokuwa na migogoro, wasikae kimya bali wapaze sauti ili wapate msaada wa kusuluhishwa na kama ikishindikana waachane na siyo kung’ang’ania na mwisho wa siku wanapigana na kutokea mauaji.

Aliwaomba pia viongozi wa dini waendelee kutoa mafundisho ya ndoa kila mara badala ya kuishia siku za kufungisha ndoa tu, sababu ndoa nyingi kwa sasa zina migogoro na zinahitaji maombi na mafundisho.

## Mbunge awapa maji wananchi wake

**Na Mathias Marwa,** MUSOMA

MBUNGE wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, amesema tatizo la maji linatarajiwa kumalizika baada ya kukamilika mradi wa bomba la maji kutoka Mugango kupitia Kiabakari hadi Butiama mkoani Mara.

Mradi huo ambao unatarajiwa kukamilika Juni 30, mwaka huu, utagharimu Sh. bilioni 70.5 kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi Barani Afrika (BADEA) na Serikali ya Saudi Arabia.

Prof. Muhongo akizungumzia mradi huo, alisema kuwa serikali ya Saudi Arabia imechangia zaidi asilimia 49.12 na BADEA 31.40.

Alisema serikali ya Tanzania imetoa Sh. bilioni 4.775 sawa na asilimia 19.48 ambazo zimeelekezwa kujenga miundombinu ya usambazaji wa maji kwenye kata za Mugango na Tegeruka, Musoma Vijijini.

Prof. Muhongo alisema kuwa choteo la maji lililojengwa katika kijiji cha Kwibara, Kata ya Mugango litakuwa na uwezo wa kuchota lita milioni 35 za maji kwa siku.

Kiwango hicho cha maji kitasaidia wananchi wengi hususani wanawake ambao ndiyo wanaopata adha kubwa ya kero ya uhaba wa maji.

Musoma Vijijini ni moja ya majimbo yenye shida ya maji licha ya kuwa karibu na Ziwa Victoria.

Mradi mwingine ambao unatarajia kuleta neema katika jimbo hilo ni ule wa kilimo cha umwagiliaji katika kata ya Bugwema, Musoma vijijini ulioridhiwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ufufuliwe katika jimbo hilo.

Mradi huo wa kilimo cha umwagiliaji ulikusudiwa na serikali ya awamu ya kwanza katika miaka ya 70 kwa lengo la kilimo cha mpunga, mahindi, dengu pamba na alizeti, lakini haukuendelezwa.

## Congo kunavyozidi kutibuka, IS yadaiwa kuua kanisani

Ukurasa 12



siasa
JUMATANO JANUARI 18, 2023
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU



Ukurasa 14

## TUNDU LISSU MIAKA 5 UGHAIBUNI...

### KUONDOKA KIFUNGONI

# Vyama vya siasa sasa ni mguu sawa, vyaanza kujadili kipengele cha masharti

**Na Sabato Kasika**

BAADA ya mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa kuruhusiwa, baadhi vimeshaianza, vingine vikiwa vinajiandaa kuanza wiki ijayo na vipo pia ambavyo vinajipanga kukutana kujadili jinsi ya kuendesha harakati za kisiasa.

CUF, imefungua pazia, ikizindua mikutano ya hadhara, Jumamosi iliyopita katika viwanja vya Bakhresa Manzese Dar es Salaam.

Uzinduzi huo unafuatiwa na kila mkoa kuandaa mikutano hiyo, huku viongozi wake wakitarajiwa kujichimbia kwa siku tatu kwenye vikao maalum kujadili mikakati ya kufanikisha mikutano hiyo.

Magdalena Sakaya Naibu Katibu Mkuu wa CUF Bara, anasema, vikao vitaanza kesho, makao makuu ya chama Buguruni Dar es Salaam na kwamba vitajadili masharti ya serikali mikutano hiyo.

"Pamoja na kuzindua mikutano yetu, lakini tumeona kuna haja ya kukutana kwanza kujadili mambo mbalimbali yakiwamo masharti ya serikali ya kutaka mikutano isiwe na matusi na kashfa," anasema Magdalena.



Magdalena Sakaya Naibu Katibu Mkuu wa CUF Bara. **PICHA:CUF**

**WATAKA UHURU**

Naibu Katibu Mkuu anaitaka serikali iache waseme ukweli katika mikutano ya hadhara, kwa kuwa wamejipanga kujenga hoja zenye maslahi kwa umma na kukosoa kwa hekima.

"Tutakosoa kwa hekima na tunaiomba serikali isitufunge midomo, ituache tuseme ukweli na ukweli usije ukaonekana kama matusi, hivyo ni muhimu kukubali ukweli na kuufanyia kazi."

Anasema chama hicho kimezindua mikutano yake Jumamosi na kwamba kila mkoa unaendelea na ratiba ya mikutano ya hadhara.

Magdalena anafafanua kuwa kuanzia kesho, vigogo wa chama hicho, watajichimbia katika vikao kwa siku tatu, kwa ajili ya kujadili mikakati mbalimbali ya kufanikisha mikutano ya hadhara.

"Tuna hoja nyingi za kupeleka kwa wananchi, kuanzia mfumuko wa bei ya vitu mbambali kikiwamo chakula, utendaji mbovu wa baadhi ya viongozi wa serikali, rushwa kukithiri, huduma mbovu za afya hospitalini na maisha magumu," anasema.

Mwanasiasa huyo anasema hakuna mpinzani ambaye anaweza kuongea kwa kupamba, bali atasema ukweli, ambao anaamini serikali ikiuchukua na kuufanyia kazi utachangia maendeleo ya nchi.

"Taifa linaongozwa kwa sheria, kanuni na taratibu, hivyo wale ambao watakwenda kinyume, wachukuliwe hatua, lakini angalizo letu ni kwamba, ukweli usigeuzwe kuwa kashfa au matusi," anasisitiza.

**ACT KUJADILIANA**

Wakati mikutano ya hadhara imeruhusiwa, Kamati Kuu cha Chama cha ACT-Wazalendo, inatarajia kukutana jijini Dar es Salaam wiki ijayo Januari 21, kujadili ajenda tatu ikiwamo programu ya ujenzi wa chama 2023.

Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Mawasiliano ya Umma wa chama hicho, Janeth Rithe, anasema watazungumzia pia hali ya kisiasa nchini pamoja na mambo mengine kuhusu ruhusa ya mikutano ya hadhara.

"Kamati Kuu itajadili pia hatua iliyofikiwa kwenye ajenda ya mageuzi ya kisiasa na kuidhinisha ratiba ya uzinduzi wa mikutano ya hadhara ya chama chetu itakayofanyika nchi nzima," anasema Janeth.

Anafafanua kuwa masuala yote yakiwamo ya jinsi ya kuendesha siasa za kistaarabu na zenye manufaa kwa umma, yatajadiliwa kwa kina na wajumbe wa kamati hiyo na kuiongeza kuwa chama chao ni chenye hoja, si vurugu.

**NI HOJA SI MATUSI**

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, anasema mikutano yao itakuwa na hoja zaidi ya 10 na si matusi.

"Tuna hoja, sera na ajenda zetu, si matusi, viongozi wasiwe na hofu. Mtu anapotoa lugha za kashfa na matusi, kuna sheria, zinaelekeza cha kufanya, viongozi wasitabiri kitakachozungumzwa katika mikutano," anaonya Mrema.

Kwa mujibu wa Mrema, ratiba ya mikutano ya chama hicho itaanza wiki ijayo, Januari 21 Mwanza, kisha Musoma mkoani Mara na kuendelea katika maeneo mengine ya Tanzania Bara na Visiwani.

"Tutarejea katika hotuba za viongozi wetu mbalimbali walizowahi kutoa kwenye mikutano ya hadhara, kwa kuzingatia kuwa mikutano ilizuiliwa si kwa sababu ya matusi bali kwa sababu ya kutaka watu wachape kazi," anasema.

Anafafanua kuwa CHADEMA si chama cha matusi bali cha hoja zenye mashiko kwa taifa na kwamba hoja zao huwa ni chungu kwa baadhi ya viongozi wa serikali ambao huzichukulia kama matusi.

Kiongozi huyo anaongeza kuwa wamechagua 21 Januari kuwa siku ya uzinduzi wa mikutano ya hadhara, kwa kuwa ni tarehe ambayo kilipata usajili wa kudumu mwaka 1993 na kitakuwa kinatimiza miaka 30.

Rais Samia Suluhu Hassan, ameanza mwaka 2023 kwa kukutana na viongozi wa vyama vya siasa, na kuridhia mambo makuu matatu katika medani za siasa, ambayo yalikuwa kilio kikubwa cha wanasiasa.

Katika mkutano huo, anaruhusu rasmi mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, lakini akisisitiza zaidi siasa za kistaarabu na kuwataka wanasiasa kuepuka kejeli na matusi.

Akizungumza katika mkutano huo anafafanua kuwa aliitisha mikutano hiyo kwa kuwa kulikuwa na masuala yaliyozungumzwa na bado hayajatolewa maamuzi, hivyo akasema ipo haja ya kufanya taifa kuwa kitu kimoja na kuwapo kwa maridhiano.

Tanzania ina vyama 19 vyenye usajili wa kudumu vinavyotarajiwa kufanya mikutano ya hadhara ambavyo ni UPDP, NRA, TADEA, TPL, CHADEMA, CUF, NCCR, UDP, UMD, CCM, Demokrasia Makini, DP, SAU, AFP, CCK, ADC, CHAUMMA na ACT- Wazelendo.



Ndivyo maisha yalivyo Congo ni silaha muda wote, kujihami, kupigana au kusalimisha kuacha uasi. **PICHA: REUTERS**

# Congo kunavyozidi kutibuka, IS yadaiwa kuua kanisani

## •Makundi 100 ya waasi yaanzisha tishio jipya

**Na Christina Mwakangale**

IKIWA ni wiki moja tangu kundi la waasi la M23 kuahidi na kutekeleza amri ya kuachia kambi ya Rumangabo na baadhi ya maeneo nchini DRC, juhudi hizo zimekutana na shambulio jipya kanisani, huku serikali ya nchi hiyo ikidai watuhumiwa ni kundi la kigaidi la Allied Democratic Forces (ADF).

Wakati serikali ya DRC, ikisema hivyo, kundi la Islamic State (IS), limekiri kuhusika katika shambulio hilo la bomu kwenye Kanisa la Pentekoste lililoko Kasindi, mashariki mwa nchi hiyo.

Watu takribani 10 wanauawa katika tukio ambalo lilitokea waamini wakienda kwenye ibada ya Jumapili iliyopita Januari 15, kwa mujibu wa maofisa nchini humo.

Pia taarifa zinasema takriban watu 39 wamejeruhiwa na Jeshi la Congo lilieleza kwamba kitendo hicho ni cha kigaidi cha ADF.

Kundi la ADF ni mojawapo ya vikundi vya waasi vinavyojulikana hasa eneo la mashariki la DRC, ukanda ambao unatajwa kuwa wa hatari zaidi nchini humo.

Jumuiya ya kimataifa imelaani hatua ya kundi hilo na mauaji ya mamia ya raia wa DRC pamoja na kushambulia huku rambirambi zikitumwa kwa familia zilizofiwa.

Ujumbe wa Umoja wa Mataifa (UN) nchini DRC, umelaani shambulio hilo wakati Msemaji wa Jeshi la DRC, Antony Mualushayi, akisema: "Ni wazi kwamba ni kitendo cha kigaidi kinachofanywa na magaidi wa ADF ambao wamepata hasara ya vita na kipigo kutoka kwa vikosi vya Jeshi vya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo".

Kasindi iko takriban kilomita nane kutoka mji wa Beni ambako ADF ina ngome, mwishoni mwa mwaka jana, mwakilishi mkuu wa Umoja wa Mataifa nchini humo, analiambia Baraza la Usalama kwamba, usalama ni moja ya changamoto kubwa inayokabili DRC.

WAASI DRC

Kundi la Waasi wa ADF, ni la wanamgambo wa Kiislamu, lilianzishwa katika miaka ya 1990 na kimsingi linahusika na malalamiko ya ndani ya Uganda.

Tangu lilipoibuka tena DRC, kwa mfululizo wa mashambulizi dhidi ya raia wa Congo na mwelekeo wa kimataifa wa kijihadi, ADF limezidi kudai mashambulizi yanayofanyika ikiyahusisha na IS.

Siku moja baada ya shambulio hilo, mshukiwa ambaye ni raia wa Kenya, amekamatwa akihusishwa na shambulio la bomu kwenye kanisa huko Kasindi katika Jimbo la Kivu Kaskazini Mashariki mwa DRC.

Msemaji wa Jeshi la Congo, Kapteni Mualushayi, anathibitisha kwamba mshukiwa huyo alikamatwa katika kituo cha mpakani cha Kasindi muda mfupi baada ya shambulio hilo.

Rais wa Congo, Felix Tshisekedi, amelaani vikali shambulio hilo na kuahidi kuwafikisha wahalifu mbele ya sheria.

HATARI MASHARIKI

Eneo la mashariki mwa DRC, limekuwa kitovu cha mapigano ambayo yamesababisha vifo vya maelfu ya watu na kuwasambaratisha wengine wengi kwa miongo takriban miwili.

Waasi wa ADF wanaendelea kuwa tishio kwa usalama wa raia wanaoishi mashariki mwa DRC. Shambulio hilo ambalo tangu wakati huo limedaiwa ni la IS inayojiita Jimbo la Afrika ya Kati (ISCAP).

Mashirika ya kiraia mashariki mwa DRC, yamesema watu zaidi ya 60 wameuawa katika kipindi cha wiki moja kutokana na mashambulio ya makundi ya waasi.

Hivi sasa, wakuu wa majeshi wa nchi za Afrika Mashariki wanakutana tena katika mji wa Mashariki wa Goma, kubuni tena kikosi cha kikanda cha kumaliza makundi hayo ya wanamgambo.

Wanatarajia kuweka sheria, vifaa na muda wa mwisho wa operesheni za kikosi hicho, licha ya kwamba hadi sasa bado haijafahamika ni lini kikosi hicho kitaanza rasmi operesheni zake dhidi ya wanamgambo watakaokiuka maagizo ya kusitisha uasi.

Kwa nchi hizo kukutana na kijadili, si awamu ya kwanza, kwani mkutano wa aina hiyo hufanyika na hata kuundwa kwa kikosi maalum cha kikanda cha kukabiliana na makundi ya wanamgambo huko Congo.

Umoja wa Mataifa, umeweka juhudi kadhaa, kupitia ujumbe wake wa walinda amani nchini humo MONUSCO na vikosi vya kikanda vya kupambana na makundi vya wanamgambo hao, bado ghasia za mauaji ya kikatili dhidi ya raia wasio na hatia zimekuwa zikiendelea kuripotiwa mashariki mwa DRC.

Mashariki mwa DRC kuna makundi zaidi ya 100 ya wapiganaji wa misituni ambao wanasababisha kukosekana usalama, mauaji na kupora mali katika eneo hilo.

Wadadisi wa kisiasa wanasema ni vigumu kwa mashambulio makubwa ya kijeshi kuwamaliza wapiganaji wa msituni, kwa kuwa wajumbe wa makundi hayo wamekuwa na mtindo wa kujificha uraiani wanapokabiliwa na mashambulio makali.

Na kwamba mashambulizi makubwa yaliyolenga kumaliza uasi wa wanamgambo wa FDLR wanaoshukiwa kufanya mauaji ya kimbari ya Rwanda ya mwaka 1994 mwishoni mwa mwaka 2019, yaliwaua baadhi ya wapiganaji wakuu wa kundi hilo, akiwamo Sylvestre Mudacumura.

Baadhi ya maofisa wakuu wa jeshi la Rwanda walisema FDLR sio tatizo, lakini sasa kundi hilo limeanza kusikika likishutumiwa kufanya mashambulizi na sasa Rwanda ikisema linashirikiana na jeshi la Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo

Kwa mujibu wa mashirika hayo, mapigano pia yalizuka Jumapili iliyopita kwenye mji wa Ituri, baada ya kuuawa kwa mwalimu wa jamii ya Lendu na kuwachochea wapiganaji wa CODECO wanaodai wanatetea kabila la Wahema kulipiza kisasi.

Wahema na Walendu, wamekuwa na mgogoro wa muda mrefu ambao hadi sasa umesababisha vifo vya mamia ya watu kati ya mwaka 1999 na 2003 kabla ya kutumwa kwa vikosi vya kimataifa kudhibiti mauaji yaliyokuwa yanatokea.

Jumatano iliyopita kuliripotiwa mashambulizi mengine kusini mwa mji wa Ituri, ambako watu kadhaa waliuawa na waasi wanaodaiwa kuwa ni wa ADF.

Shambulio jingine la waasi wa ADF liliripotiwa Alhamisi, huku miili ya watu 21 ikipatikana kaskazini mwa Ituri, kwa mujibu wa ripoti za UN zaidi ya makundi ya waasi 120 yanafanya shughuli zao mashariki mwa DRC, mengi yakipigania kuchukua maeneo yenye utajiri wa rasilimali ikiwamo madini.

> Ujumbe wa Umoja wa Mataifa (UN) nchini DRC, umelaani shambulio hilo wakati Msemaji wa Jeshi la DRC, Antony Mualushayi, akisema: "Ni wazi kwamba ni kitendo cha kigaidi kinachofanywa na magaidi wa ADF ambao wamepata hasara ya vita na kipigo kutoka kwa vikosi vya Jeshi vya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo".

RUHUSA MIKUTANO

# Wananchi wanapongojea tena ujio hoja za upinzani

## •M4C, Operesheni Sangara kuamsha shangwe




Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, kwenye harakati za kufikisha hoja za M4C kwa wananchi. **PICHA: CHADEMA**

**Na Restuta James**

CHADEMA na vyama vingine vya upinzani vimekuwa 'jela' kwa takribani miaka saba sasa, vikifungiwa kuendesha shughuli za kisiasa kwa maelezo kuwa uchaguzi umemalizika na sasa ni kuchapa kazi si muda wa siasa tena.

Ni msimamo uliosimamiwa na awamu ya tano, ambao umesahihishwa na awamu ya sita na sasa ni ruksa kuendeleza harakati za kisiasa ikiwamo mikutano, kampeni, ziara mikoani na kukutana na wanachama.

Wakati zuio hilo lilipotangazwa rasmi itakumbukwa, Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kiliendesha operesheni kadhaa kupitia mikutano ya hadhara ambayo ilikijenga na kukitambulisha chama hicho vya kutosha kwa umma.

Mwaka 2009 kulikuwa na Operesheni Sangara ambayo ilikijenga kikamilifu chama hicho kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 na ile ya vuguvugu la mabadiliko maarufu kama M4C Pamoja Daima iliyoitangaza CHADEMA kuelekea uchaguzi wa 2015.

M4C ilikuwa na agenda tisa zikiwamo za kuona kuwa kunakuwa na maboresho ya daftari la wapigakura na katiba mpya husasani pendekezo la muundo wa serikali tatu kama ilivyokuwa imeainishwa na Tume ya Jaji Joseph Warioba.

Katika operesheni hizo viongozi wakuu wa CHADEMA waligawana katika mikoa mbalimbali na hivyo kazi ya kufikisha hoja zake kwa wananchi na wanachama ilifanyika ndani ya muda mfupi na kwa ufanisi mkubwa, kwa mujibu wa maelezo ya Mwenyekiti Freeman Mbowe.

> Katika operesheni hizo viongozi wakuu wa CHADEMA waligawana katika mikoa mbalimbali na hivyo kazi ya kufikisha hoja zake kwa wananchi na wanachama ilifanyika ndani ya muda mfupi na kwa ufanisi mkubwa, kwa mujibu wa maelezo ya Mwenyekiti Freeman Mbowe.

Ilikuwa ni kawaida kwa wana CHADEMA kila wanapotangaza operesheni au mikutano ya hadhara kunatajwa kuteka hisia za Watanzania hasa vijana kwa muda kutokana na namna wananchi wanavyojitokeza kwa wingi na namna wanavyopanga hoja.

Wakati wa M4C CHADEMA iliwahi kufanya mikutano ya hadhara zaidi ya 87 katika mikoa mbalimbali ndani ya wiki moja. Chama hicho kilifanikiwa kufanya mikutano mingi ndani ya muda mfupi kutokana na kwamba viongozi wakuu na wajumbe wa Kamati Kuu waligawana kanda na mikoa na kutimiza azma hiyo.

Mathalani, wakati timu ya Mwenyekiti wa CHADEMA Mbowe, ikiwa mkoani Geita, Tundu Lissu na kikosi chake walikuwa Dodoma na Godbless Lema, alikuwa Bukoba kueleza hoja za M4C na kuwafafanulia wananchi kile wanacholenga.

Hata hivyo, hoja kama ya katiba mpya pamoja na suala la Tume Huru ya Uchaguzi bado hazikupatiwa ufumbuzi hivyo ni wazi kwamba kwenye mikutano ya chama hicho haitakosekana, kuibuka na kujadili upya kwa kuzingatia ahadi ya sasa ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kutaka maridhiano na ustahimilivu

Ndiyo ruhusa ya mikutano ya hadhara ambayo ni kama iliondolewa kwa takribani muongo mzima sasa hivyo ndiyo fursa ambayo itawapa wananchi na husussani wafuasi wa vyama vya upinzani wasaa wa kujadili masuala muhimu ya taifa kama taarifa mbalimbali za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na matumizi ya fedha za umma, deni la taifa, miradi ya maendeleo na mwelekeo wa kiuchumi wa nchi na dunia.

Kadhalika, kupanda kwa bei za vyakula na bidhaa mbalimbali muhimu kama mafuta na usafirishaji na jinsi unavyoathiri maendeleo.

Pia wananchi watapata nafasi ya kuwasilisha hoja zao ambazo mara nyingi huziwasilisha kwa njia ya mabango.

Ndiyo maana kila mwenye kupenda ustawi na maendeleo ya kidemokrasia anapongeza hatua hii ya Rais Samia Suluhu Hassan, kwani ni kama njia ya kukipa tena nafasi chama chake CCM kusikia kutoka kwa wananchi.

Pia suala la kuendelea kupanda kwa deni la taifa halitakwepeka kwenye mikutano ya hadhara ya Chadema na ya vyama vya upinzani kwa ujumla.

Hili litakwenda sambamba na kuangazia upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii hususani kwenye sekta za elimu, afya, maji na kilimo.

Kwenye sekta ya elimu, pamoja na kwamba serikali inapeleka ruzuku kwenye shule za msingi na sekondari, bado kuna upungufu mkubwa wa madarasa na madawati na uchambuzi wa kina unafanywa na upinzani kuiwezesha serikali kujisahihisha.

Ni kawaida kwenye shule za umma kwa wanafunzi kukaa chini hadi mbele chini au karibu na ubao kutokana na kwamba idadi yao ni kubwa darasani.

Kadhalika, shule nyingi za umma zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa walimu jambo ambalo linalosababisha ufundishaji kuwa mgumu.

Kwenye sekta ya afya changamoto hazitofautiani sana na zile za elimu kwani kuna upungufu wa majengo, vifaa tiba na dawa pamoja na wataalamu.

Ni kawaida kukuta zahanati ya umma inayohudumia takribani wagonjwa zaidi ya 300 kwa siku ikiwa na mtaalamu mmoja wa maabara, daktari mmoja au wawili na mfamasia mmoja, lakini pia kutokana na mzigo wa kazi si rahisi kuwakuta wote kazini kila siku.

Hayo ni miongoni mwa mambo ambayo wapinzani wanatakiwa kuyachunguza na kuishauri serikali nini cha kufanya na kuweka bayani wapi kwenye upenyo wa kuboresha maisha ya Watanzania.

Upungufu wa wataalamu kwenye hospitali za umma unachangia kiasi kikubwa kero kwa wagonjwa kwani wanasubiri muda mrefu kupata huduma katika hatua zote kuanzia kumwona daktari, kufanyiwa vipimo hadi kupata tiba.

Suala la upatikanaji wa majisafi na salama kwa wananchi wengi mjini na vijijini linafanyiwa kazi lakini juhudi zaidi zinahitajika ni hoja ambayo inatazamiwa kuandikwa kwenye mabango na kutolewa kwa viongozi wa upinzani, ili kuihamasisha na kuichochea serikali kuongeza juhudi.

Kadhalika, upatikanaji wa pembejeo za kilimo kama mbolea na mbegu ni hoja ambayo hata isipoibuliwa na vyama kwenye mikutano ya hadhara, wananchi wataisema kupitia mabango, mitandao ya kijamii na vijiweni.


Hii ni kwa sababu kilimo kinagusa asilimia 75 ya maisha ya Watanzania. Kuna suala serikali kuchukua sehemu ya mashamba ya wananchi na kuyarejesha kwenye hifadhi za taifa kama ilivyotokea wilayani Mbarali, mkoa wa Mbeya kwenye mashamba ya mpunga.

Ni wakati wa upinzani kutumia hoja za kisiasa, kuishauri na kuikosoa serikali kuangalia na kuharakisha kasi ya maendeleo.

# TUNDU LISSU MIAKA 5 UGHAIBUNI...

## •"Ni furaha kuibusu tena ardhi ya Tanzania"
## •Kuingia rasmi saa 7:35 mchana Jumanne

**Na Mwandishi Wetu**



Rais Samia Suluhu, kwenye mkutano na Tundu Lissu.

KIONGOZI wa upinzani aliyenusurika kifo baada ya kumiminiwa risasi nyingi, Tundu Lissu, anatarajiwa kurejea nchini kuanzia wiki ijayo, baada ya kuishi ughaibuni kwa takriban miaka mitano sasa.

Mwanasheria msomi na Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Bara, Lissu ambaye alipata hifadhi ya kisiasa nchini Ubelgiji, anasema anarudi Tanzania kutokana na kile anachokieleza kuwa ni mazingira ya kisiasa yanayoimarika baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuchukua uongozi wa nchi, Machi 2021. Anaeleza hayo anapozungumza na vyombo vya habari vya kimataifa.

Ni rasmi kuwa Lissu anarudi, kama anavyonukuliwa John Mrema, Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itikadi na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, akisema wananchi watatangaziwa.

Lissu anaahidi kuibusu ardhi ya Tanzania kwa mara nyingine tena Januari 25, 2023, saa 7:35 mchana na Shirika la Ndege la Ethiopia kutoka Addis Ababa, namba ET 805.

"It's now official: I'll be kissing Tanzanian soil once again on Wed. 25 Jan., 2023, at 13:35 hrs local time. I'll arrive aboard Ethiopian Airlines #ET805 from Addis Ababa. With the lifting of the illegal ban on political activity, it's now time to return home & get back to work!" Aliandika kwenye mtandao wa twita saa 1:35, Januari 13, 2023.·

Anasema kinachompa nguvu ni kuondolewa kwa marufuku ya mikutano ya kisiasa na kuruhusiwa shughuli zinazohusisha mikutano na anaona kuwa ni wakati wa kurejea nyumbani na kufanya kazi za kisiasa.

**KUPIGWA RISASI**

Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Lissu, alinusurika jaribio la kuuliwa baada ya kupigwa risasi 16 mwaka 2017 akiwa kwenye makazi ya wabunge Dodoma.

Septemba 2017 wakati kikao cha bunge kikiendelea Dodoma watu wasiofahamika wenye silaha walimfyatulia risasi nje ya nyumba yake ikidaiwa kuwa ni baada ya kumfuata mbunge huyo wa upinzani wakati huo akiwa anatoka kwenye shughuli za kikazi bungeni.

Akiwa amekaa bungeni kwa miaka michache kuanzia Novemba 2015 hadi Septemba 2017, Lissu, aliyewahi kuwa Rais wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), alielezwa kuwa alikuwa akielekea nyumbani kwake saa 5:00 asubuhi baada ya shughuli za bungeni na hapo alibaini kuwa kuna magari mawili yalikuwa yakimfuata.

Kila alipogeuza au kupunguza mwendo, magari hayo ambayo yalidaiwa kuwa ni aina ya Nissan nyeupe na Land Cruiser yalikuwa yakifuata njia au kila hatua gari lake lililochukua na kuongeza wasiwasi.

Hata hivyo alikuwa anaishi kwenye nyumba ya serikali na mahali wanapoishi mawaziri na viongozi wengine wa serikali alipopaeleza kuwa ni salama kila wakati na kulikokuwa na ulinzi muda wote.

Baada ya kujeruhiwa jaribio la mauaji mjini Dodoma, Lissu alikimbizwa nchini Kenya kwa ndege ya kukodi kutoka kwenye kampuni ya mbunge wa zamani wa Mpendae -Zanzibar mfanyabiashara maarufu Salim Turky, sasa ni marehemu.

Lissu alilazwa na kupata matibabu jijini Nairobi lakini alihitaji tiba zaidi na kupelekwa Ubelgiji kwa matibabu ya kibingwa na kuendelea kuishi nchini humu tangu 2017.

Wakati akipata masahibu hayo Lissu alikuwa mbunge wa Singida Mashariki kwa tiketi ya CHADEMA na Mnadhimu Mkuu wa Upinzani bungeni.

Juhudi za kuokoa maisha yake zilifanikiwa kwa upasuaji wa raundi nyingi, kuunga na kuunda mifupa yake mara kadhaa, huko Ubelgiji baada ya kupigwa risasi 16 mfululizo na kupoteza damu nyingi na kuharibika mifupa ya mguu mmoja ambao baada ya matibabu umekuwa mfupi ukilinganishwa na mwingine.

Alikuwa akiishi uhamishoni katika mji wa Tienen nchini humo ulio takribani kilometa 50 nje ya jiji la Brussels.

Lissu anatangaza kurudi nyumbani akikiri kuwa yuko tayari kwa mwanzo mpya wa safari ya kisiasa ya Tanzania inayojumuisha mchakato wa kupata katiba mpya na harakati za siasa za vyama vya upinzani.

Anasema kama raia wanaowajibika, anaitikia wito wa Rais na kunaonyesha utayari wao kwa safari hiyo akiahidi kurudi nyumbani kwa ajili ya kazi iliyo mbele yake ambayo ni kushiriki kwenye mchakato wa katiba na mwanzo mapya kwa mustakabali wa Tanzania.



Tundu Lissu akijiandaa kurejea nyumbani. **PICHA: MTANDAO**

**KUGOMBEA URAIS**

Oktoba 2020, Tundu Lissu alirejea nchini na kugombea urais kwa tiketi ya CHADEMA, akichuana vikali na mgombea wa CCM, John Magufuli, kwenye uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28.

Hata hivyo, baada ya matokeo kutangazwa ambako Magufuli alirudishwa tena ikulu Oktoba 28 kwa asilimia 84 ya kura zote, alirejea tena Ubelgiji alikotibiwa majeraha mengi ya risasi, mivunjiko ya mifupa na kuchanika misuli na mishipa mingi na kunusurika kifo katika tukio ambalo hadi leo, haifahamiki ni nani walikuwa watesi wake.

Kwenye uchaguzi huo ambao wapinzani Tanzania Bara walipata viti viwili vya ubunge, Magufuli alipata kura zaidi ya milioni 12.5 wakati Lissu akiambulia takribani milioni 1.9.

Baada ya kushindwa na kurudi uhamishoni Lissu, hata hivyo, hakukata tamaa ya kupigania demokrasia, akieleza kuwa kinachompa nguvu ni kuungwa mkono kwa kiasi kikubwa alipokuwa kwenye kampeni.

Anaahidi kuwa atarudi tena Tanzania japo hakujua ni lini akieleza kuwa hawezi kubaki Ulaya milele na kwamba jambo muhimu zaidi kwake ni kuendeleza mapambano na utetezi wa demokrasia bila kujali.

Lissu alianza kuahidi kurejea nyumbani akisema itatokea mara baada ya kuhakikishiwa usalama wake. Alitangaza hayo baada ya kukutana na Rais Samia Suluhu Hassan jijini Brussels, alikokuwa ameishi uhamishoni tangu aliponusurika jaribio la mauaji mwaka 2017.

Tundu Lissu, mwanasheria na mtetezi wa haki za binadamu na mmoja wa viongozi maarufu wa upinzani nchini ana sifa ya 'kuchonga' na mara nyingine anaweza kusema bila kujali, kwa mfano alikuwa akitumia jina 'dikteta uchwara' kuponda uongozi wa awamu ya tano.





## Awamu ya pili majengo ofisi za wizara kukamilika kabla Oktoba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

UJENZI wa awamu ya pili ya majengo ya kudumu ya ofisi 26 za wizara yanayojengwa katika Mji wa Serikali Mtumba jijini hapo, umefikia asilimia 70 na unatarajiwa kukamilika kabla ya Oktoba, mwaka huu.

Aidha, serikali imekamilisha ratiba na mwongozo utakaowezesha taasisi za serikali ambazo bado zinaendelea kutekeleza majukumu yake Dar es Salaam kuhamia Dodoma.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, aliyasema hayo juzi jijini hapo kwenye hafla ya kukabidhi vibali vya ujenzi wa ofisi za taasisi Dodoma.

Simbachawene alisema ujenzi wa majengo hayo unagharimu Sh. bilioni 675.

Kuhusu taasisi, Waziri Simbachawene alisema serikali ilikuwa na taasisi 189 zilizokuwa zinatekeleza majukumu yake jijini Dar es Salaam na kutokana na serikali kuhamishia shughuli zake Dodoma, taasisi 55 za serikali zimetekeleza maelekezo hayo kwa kuamua kujenga ofisi zake Dodoma.

"Hadi sasa taasisi 20 zimekamilisha ujenzi, 16 zinaendelea na hatua mbalimbali za ujenzi. Nyingine 19 zipo katika maandalizi ya kuanza ujenzi baada ya kupata vibali vya ujenzi kutoka kwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa," alisema.

Hata hivyo, alisema katika kutekeleza ratiba na mwongozo wa taasisi kuhamia

Dodoma kwa awamu, Waziri Mkuu ametoa maelekezo kwa taasisi 42 zihamie ndani ya mwaka wa fedha 2022/23.

"Taasisi 36 zitahamia Dodoma katika mwaka ujao wa fedha wa 2023/24 na 19 zitahamia katika mwaka 2024/25 wakati taasisi 27 zimeelekezwa kwa kuzingatia aina ya majukumu zilizonazo mkoani Dar es Salaam. Hatua hii itakamilisha sehemu kubwa ya Mpango wa Serikali wa kuhamia Dodoma ambapo hadi sasa tayari taasisi 65 zilishahamia Dodoma tangu mwaka 2016 hadi 2022," alisema.

Alitoa wito kwa taasisi zote zinazoendelea na ujenzi Dodoma unakamilika kwa kuzingatia taratibu zote ikiwamo ubora, muda, bajeti iliyotengwa na thamani ya fedha ili kuleta tija inayotarajiwa.

"Taasisi nyingine ambazo bado hazijaanza maandalizi ya ujenzi Dodoma ziwasilishe Ofisi ya Waziri Mkuu mahitaji ya viwanja vya ujenzi wa ofisi za taasisi Dodoma kwa ajili ya uratibu wa pamoja," alisema.

# TALGWU yataja kero zinazoumiza wanachama

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) kimetaja kero nne zinazowaumiza wanachama wao nchini ikiwamo malipo ya waliofukuzwa kazi kwa vyeti feki.

Mkuu wa Idara ya Habari ya Mahusiano wa chama hicho, Shani Kibwasali, aliwasilisha kero hizo juzi alipokuwa akisoma risala ya chama hicho kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenister Mhagama, kwenye mkutano mkuu wa chama hicho uliofanyika jijini hapo.

Kibwasali alizitaja kero hizo kuwa ni kushushwa mishahara kwa watumishi ambao baada ya kutoka kujiendeleza kielimu na kuomba kubadilishiwa kada huku akiwa ameshafanyakazi kwa muda mrefu.

Alisema mtumishi huyo akitaka kubadilishiwa kada kwa sasa ashushwa mshahara kulingana na kada mpya aliyoingia na kuiomba serikali kuangalia upya suala hilo ambalo linaonekana ni kulinyima haki kundi hilo.

Aliitaja kero ya pili kuwa ni baadhi ya watumishi wenye elimu ya darasa la saba waliondolewa kazini mwaka 2017 kwa kosa la cheti na baadaye kurejeshwa kazini Aprili 2018 wengi wao hawajalipwa fedha zao za mishahara.

Alisema chama hicho kinamwomba Waziri Mhagama kuziagiza mamlaka husika kutekeleza agizo la serikali lililotolewa bungeni ili wanachama wao walipwe haki zao.

"Kero nyingine ni baadhi ya halmashauri kutoitisha vikao vya mabaraza ya wafanyakazi kwa mujibu wa sheria pamoja na yale yaliyomaliza muda wake mwaka jana, hadi kufikia Desemba 2022 kati ya halmashauri 196 ni 156 zenye mabaraza hai ya wafanyakazi," alisema.

Aidha, mabaraza hayo yanatakiwa kufanya vikao mara mbili kwa mwaka kwa mujibu wa sheria ili wafanyakazi wakae na mwajiri wao kujadiliana mambo ya kikazi na stahiki zao.

Kero nyingine aliyoitaja ni wanachama wao wa kada ya maofisa watendaji kukabiliwa na matatizo ya matumizi ya mashine za kukusanya mapato jambo ambalo linawasababishia kukutwa na makosa ya kiutumishi na kijinai.

Aliwaomba wakurungenzi wa halmashauri kutoa mafunzo ya kutosha kwa kada hiyo ya matumizi sahihi ya mashine hizo za kukusanya mapato ili kuepuka kuingia kwenye makosa yanayowaondoa kazini.

Mwenyekiti wa TALGWU Taifa, Tumaini Nyamhokya, alisema jukumu la mkutano mkuu huo ni kupitisha taarifa za utekelezaji wa shughuli za chama kwa mwaka 2022.

Alisema pia jukumu lingine ni kupitisha makisio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023 pamoja na kufanya uchaguzi wa nafasi ya Naibu Mkuu wa TALGWU Taifa.

Waziri Mhagama aliwataka wafanyakazi nchini kutekeleza wajibu wao bila hofu kwa sababu serikali ni sikivu na imeanza kuzifanyia kazi baadhi ya kero.

Alisema watakaa na wizara zingine ili kutatua kero na malalamiko ya kushushwa mishahara kwa sababu ni haki ya mtumishi kujiendeleza kielimu.

Aidha, serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni 58 kwa ajili ya kulipa watumishi waliopanda madaraja na kuhusu wafanyakazi walioondolewa kazini na kurudishwa kazini serikali iliagiza walipwe na kuwataka waajiri wahakikishe wanatekeleza.

Pia, wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuruhusu vikao vya mabaraza ya wafanyakazi kufanyika mara mbili kwa mwaka kwa kuwa ni takwa la kisheria.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama (katikati), akiwa na Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) Taifa, Tumain Nyamhokya (kushoto) na Makamu Mwenyekiti, Romward Mwashiuya, wakishiriki kuimba wimbo wa mshikamano wakati wa kufungua mkutano mkuu wa chama hicho jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wazazi wadaiwa kuwageuza watoto walinzi wa nyumba kipindi cha kilimo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

DIWANI wa Kata ya Msalato jijini Dodoma, Nsubi Bukuku, amesema wazazi na walezi katika kipindi cha kilimo wanawageuza watoto wao walinzi wa nyumba badala ya kuwapeleka shule.

Bukuku alitoa wito huo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu shule mpya ya msingi ya Msalato iliyojengwa na serikali na nguvu za wananchi katika kata hiyo iliyofunguliwa mwishoni mwa wiki.

Alisema, wazazi na walezi wenye watoto walioandikishwa kuanza masomo wanatakiwa kuwapeleka shule ili wasome na sio kuwaacha majumbani na kuwageuza kuwa walinzi wa nyumba.

"Kilimo kisiwe kikwazo cha kutowapeleka watoto hao shuleni kwa wale walioandikishwa ili kuanza masomo," alisema.

Aliwataka kutoa ushirikiano kwa serikali ili watoto hao wafanye vizuri kitaaluma na kuwezesha shule hiyo kuwa mfano wa ufaulishaji kwa wanaomaliza elimu ya darasa la saba.

Alisema ushirikiano huo utawawezesha kufanya vizuri kitaaluma kwenye shule hiyo mpya iliyojengwa kutokana na iliyokuwapo kubomolewa kwa ajili ya kupisha mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato.

"Shule hii ni mpya imejengwa hapa baada ya ilipokuwa hapo awali kupitiwa na ujenzi wa uwanja mpya wa ndege wa kimataifa, hivyo niwaombe wazazi na walezi wasiwe kikwanzo cha kuwakwamisha na badala yake wawe karibu kuwafuatilia kwenye masomo ili waweze kufanya vizuri kitaaluma," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Msalato, Emmanuel Mazengo, aliwataka wazazi na walezi kushirikiana na serikali katika kuilinda na kutunza mazingira ya shule hiyo ambayo imejengwa kwa gharama kubwa na fedha za serikali.

Mazengo aliwataka wazazi na walezi kuhakikisha wanashirikiana kwa pamoja na serikali katika kuitunza na kuilinda ili mazingira ya shule hiyo yasiharibiwe na watu pamoja na mifugo.

Augustino Mwimbe mmoja wa wazazi wa kata hiyo ya Msalato alisema kuwa ili ufaulu wa watoto uwe mzuri na kufikia malengo yao kuna umuhimu wa kuwapatia mahitaji yao ya kimsingi yanayohitajika kwenye upande wa elimu.





# Serikali yaridhia subira ya wananchi kuondoka hifadhini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeridhia ombi la wananchi wa vijiji vitano vya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya vilivyoondolewa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha la kutaka kuendelea kuhudumia mazao yao mpaka watakapovuna ndipo waondoke kupisha shughuli za uhifadhi.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliyasema hayo juzi jijini Mbeya alipozungumza na wadau mbalimbali wa maendeleo kutoka wilayani Mbarali kuhusu shughuli mbalimbali za maendeleo katika wilaya hiyo zikiwamo shughuli za uhifadhi.

Wadau walioshiriki kikao hicho ni pamoja na wafugaji, wakulima, wawekezaji wa mashamba ya serikali, wamiliki wa viwanda vya kuchakata mpunga na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo na mifugo.

Aidha, katika kikao hicho pia walihudhuria mawaziri na manaibu waziri wa wizara nane za kisekta waliokuwa wanashughulikia mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) na maofisa wa Bonde la Maji la Mto Rufiji.

Waziri Mkuu alisema katika mapitio ya mipaka ya hifadhi hiyo walibaini kuwa maeneo ya vijiji vilivyoondolewa bado yana tija kwenye uhifadhi na hivyo wakaamua kuviondoa ili kulinda rasilimali zilizoko.

Alisema Wilaya ya Mbarali ni muhimu kwa maendeleo ya taifa kutokana na kuwa chanzo cha maji yanayotumika kwenye shughuli mbalimbali za uchumi lakini inakabiliwa na tatizo la uharibifu wa mazingira ambalo linatishia uendelevu wa maji hayo.

Alisema wilaya hiyo ina idadi kubwa ya mifugo isiyoendana na mahitaji jambo ambalo linachangia uharibifu wa mazingira pamoja na migogoro ya wafugaji na hifadhi pamoja na migogoro ya wafugaji na wakulima.

Vilevile alisema kuna kilimo cha umwagiliaji kisichokuwa endelevu ambacho pia kimekuwa kikisababisha uharibifu wa mazingira hasa uchepushaji wa maji kwa ajili ya umwagiliaji bila kuwa na vibali.

"Timu ya mawaziri wetu wanane imefanya kazi nzuri sana ya kushughulikia mgogoro baina ya wananchi na hifadhi yetu, wamerekebisha mipaka ya GN (28) (Tangazo la gazeti la serikali namba 28 la mwaka 2008) ambapo ni vijiji vitano pekee ndivyo vinalazimika kuondolewa kwa sababu vipo kwenye maeneo nyeti," alisema Majaliwa.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Pindi Chana, alipiga marufuku wafugaji kuingiza tena mifugo kwenye maeneo waliyoondolewa, huku akitahadharisha kuwa hatua kali zitachukuliwa kwa watakaokamatwa ndani ya maeneo hayo.

Alisema mifugo yote itakayoendelea kukamatwa ndani ya hifadhi itataifishwa kwa mujibu wa sheria ili iwe fundisho kwa wengine wenye nia ya kuingiza mifugo hifadhini.

"Sheria inaturuhusu kutaifisha mifugo inayokutwa ndani ya hifadhi, kwa hiyo nawaomba wafugaji mzingatie sheria, mfuge kwa tija ili msije mkaingia hasara ya mifugo yenu kutaifishwa," alisema Waziri Chana.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema kwa sasa wanaendelea kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu kuboresha ufugaji kwa kupunguza idadi ya mifugo na kufuga kwa tija ili kuondokana na migogoro isiyokuwa na sababu.

Alisema lengo la wizara ni kuondokana na wafugaji kuchunga na badala yake wafuge ili kupunguza migogoro ambayo imekuwa ikijitokeza mara kwa mara.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, alisema maji yanayotokana na vyanzo vya maji vilivyoko Mbarali ni muhimu kutokana na kuwa vyanzo vya uzalishaji wa nishati kwenye Bonde la Rufiji.

Alisema katika kipindi cha uongozi wake atahakikisha Mto Ruaha unaendelea kutiririsha maji mwaka mzima ili miradi inayojengwa na serikali iwe na tija.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na wadau waliowekeza katika Bonde la Usangu, ikiwamo wakulima wa mpunga na wafugaji jijini Mbeya juzi. **PICHA: OWM**

# TFS yaomba kuupandisha hadhi Msitu wa Hifadhi Kipembawe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) imeomba kuupandisha hadhi Msitu wa Hifadhi wa Kipembawe uliopo wilayani Chunya na kuwa Hifadhi ya Nyuki ili kuzuia uharibifu wa mazingira ambao umekuwa ukisababishwa na shughuli za kibinadamu.

Aidha, mamlaka hiyo imesema lengo lingine la kuomba kupandishwa hadhi kwa msitu huo ni kuongeza kiwango cha uzalishaji wa mazao ya nyuki ikiwamo asali kutokana eneo hilo kuwa na viashiria mbalimbali vinavyovutia ufugaji wa nyuki. Ofisa Nyuki wa TFS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Jane Kihwele, aliwasilisha ombi hilo kwa niaba ya Kamanda wa Kanda kwenye Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Mbeya ambapo alisema msitu huo una miti yenye asili ya miyombo ambayo inafaa kwa ufugaji wa nyuki.

Alisema msitu huo una ukubwa wa hekta 20,728 na unapatikana kilomita 146 kutoka Chunya Mjini na zaidi ya kilomita 200 kutoka Mbeya Mjini.

Alisema kupandishwa hadhi kwa msitu huo kutasaidia kuhifadhi bioanuai ya nyuki asilia, miti na wanyama pamoja na kuhifadhi wanyama wanaohama kutoka upande mmoja kwenda mwingine hasa kutoka kwenye maporomoko ya Rukwati na Piti.

Alisema wameshafuata taratibu zingine ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wananchi wa vijiji vinavyozunguka pori hilo pamoja na Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

"Hatua zote muhimu tumeshazifanya na ramani imeshaandaliwa ya eneo husika, msitu huu ni muhimu kwa sababu unaweza ukatumika kama eneo la mafunzo kwa vitendo kuhusu ufugaji wa nyuki," alisema Jane.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde, alikiri halmashauri yake kupokea na kuridhia maombi ya TFS kutokana na umuhimu wa eneo hilo.

Alisema maofisa wa TFS walieleza umuhimu wa kupandishwa hadhi kwa msitu huo huku akisisitiza kwamba madiwani na wadau wengine walishirikishwa na wao wakaridhia.

Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Mbeya, iliridhia ombi hilo la TFS na kuagiza shughuli za ufugaji wa nyuki kuanza haraka ili kuongeza kiwango cha uzalishaji wa mazao ya nyuki.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka maofisa wa TFS kushirikiana na vijiji vya Mazimbo na Mafyeko kulinda msitu huo ikiwa ni pamoja na kuzuia moto ambao umekuwa ukiteketeza misitu na rasilimali zilizomo.

## Taasisi, watu binafsi waitwa kuwasaidia waathirika mafuriko

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMATI ndogo ya maafa ya Mkoa wa Mbeya inayoratibu ukusanyaji wa michango ya watu waliopata maafa kutokana na mafuriko katika Kata ya Uyole jijini Mbeya imewaomba wadau mbalimbali zikiwamo taasisi na watu binafsi kuwasaidia waathirika.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Erick Sichinga aliyasema hayo juzi wakati akipokea msaada wa nguo kutoka taasisi isiyo ya kiserikali ya Sauti ya Mama Afrika (SAMAFO) kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maafa Mkoa ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera.

Alisema pamoja na serikali kuwasaidia waathirika hao mahitaji mbalimbali bado uhitaji ni mkubwa kutokana na athari walizopata akieleza kuwa wengi wao hawakuweza kuokoa kitu chochote.

"Tayari Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na mkoa ilishatangulia kutoa msaada wa mahitaji mbalimbali kwa waathirika wa mafuriko lakini bado msaada huo hautaweza kutosheleza kwa muda mrefu," alisema Sichinga.

Alilishukuru Shirika la SAMAFO kwa kuwa taasisi ya kwanza kusaidia waathirika hao huku akiainisha mahitaji yanayohitajika ni pamoja na chakula, mavazi, vifaa kwa ajili ya kulalia, samani za ndani pamoja na mahitaji mengine.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Sauti ya Mama Afrika (SAMAFO), Tabitha Bugali, alisema walisikia taarifa kutoka kwenye vyombo vya habari juu ya uwapo wa mafuriko na waathirika waliokubwa na adha hiyo kuhitaji msaada hivyo walichangisha fedha.

"Shirika letu halina wafadhili lakini tunafanya shughuli mbalimbali za kijamii kwa kujitolea, hivyo tulipopata taarifa hii kwenye vyombo vya habari, mimi na wenzangu tukajichangisha fedha na kwenda kununua mavazi kwa ajili ya wanawake, watoto pamoja na vijana walioathirika na mafuriko hayo," alisema Bugali.

**Alisema pamoja na serikali kuwasaidia waathirika hao mahitaji mbalimbali bado uhitaji ni mkubwa kutokana na athari walizopata akieleza kuwa wengi wao hawakuweza kuokoa kitu chochote.**



# Matukio ya ukatili, udhalilishaji 1,360 yaripotiwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

MATUKIO 1,360 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa Zanzibar kwa mwaka 2022, kati ya takwimu hizo watoto wa kike wanaongoza kwa kufanyiwa vitendo hivyo.

Takwimu hizo zilitolewa jana na Ofisa kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Kitengo cha Makosa ya Jinai, Ramla Hassan Pandu, wakati akiwasilisha taarifa ya matukio ya udhalilishaji kwa mwaka 2022.

Alisema katika matukio hayo waathirika 1,361 wamefanyiwa ukatili huo, kwamba watoto ni 1,173, wanawake ni 185 na wanaume watatu.

Alisema watoto wa kike walidhalilishwa walikuwa 889 sawa na asilimia 75.8 na wanaume 284 sawa na asilimia 24.2.

Pandu alisema Wilaya ya Magharib B Unguja imeripotiwa kuwa na matukio mengi ikilinganishwa na wilaya zingine, matukio yalikuwa 288 ikifuatiwa na Wilaya ya Mjini yenye matukio 279.

"Wilaya ya Micheweni Pemba imeripotiwa kuwa na idadi ndogo zaidi ya matukio kuliko wilaya zote ambapo yalikuwa 39," alisema.

Aidha, alisema idadi hiyo ya matukio kwa mwaka huo yameongezeka kwa asilimia 11.3 kutoka matukio 1,222 kwa mwaka 2021 hadi 1,360 kwa mwaka 2022.

Alisema watoto 1,173 waliofanyiwa ukatili huo wasichana waliobakwa walikuwa 585, wavulana 197, wasichana walioingiliwa kinyume na maumbile 84, kutoroshwa 78 na mvulana aliyetoroshwa ni mmoja, shambulio la aibu 91, shambulio la kawaida ni 137.

Alisema idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwaka 2022 yameongezeka kwa asilimia 9.8, kwamba matukio yalikuwa 1,173 ukilinganisha na mwaka 2021 yalikuwa 1,068.

"Idadi ya watoto waathirika zaidi ni wenye umri wa miaka 15 hadi 17 wakifuatiwa na watoto wenye miaka 11 hadi 14," alisema.

Pindu alisema washtakiwa 104 wa matukio hayo kwa mwaka 2022 wamehukumiwa vifungo na wapo gerezani wanatumikia adhabu, kwamba waliobaka ni 52 na waliolawiti 18.

Hata hivyo alisema washtakiwa 784 wa matukio hayo kwa mwaka huo wapo mahabusu, kwamba wanaodaiwa kubaka ni 322, kulawiti 135, kuingilia kinyume na maumbile 111, kutorosha 69, kukashifu 89, shambulio 51 na kumwingilia kimwili maharimu nane.

Ramla alisema matukio hayo ya mwaka yaliyoripotiwa matukio 181 watuhumiwa wametiwa hatiani, kesi 139 wameachiwa huru, 421 wamefikishwa mahakamani, 534 zipo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi, 19 hakuna mtuhumiwa aliekamatwa, 64 hakuna hatua iliyochukuliwa na mawili yapo katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Mkurugenzi wa Jinsia na Watoto, Siti Abasi Ali, alisema juhudi za pamoja zinahitajika katika kutokomeza vitendo hivyo.

Alisema bado elimu kwa jamii inahitajika kupambana na vitendo hivyo na kuwataka viongozi wa dini kuendelea kutoa mahubiri katika nyumba za ibada na mikusanyiko.

Aidha, alisema lazima wazazi na walezi wafuatilie mienendo ya watoto wao kwa sababu wadhalilishaji ni watu wa karibu katika familia.

Mkaguzi wa Jeshi la Polisi, Said Ali Said alisema takwimu hizo za udhalilishaji ni za kusikitisha, hivyo juhudi zaidi zinahitajika kuwafichua wahalifu wa matukio hayo na kuitaka jamii kuacha muhali.

Mrakibu Msaidizi kutoka Jeshi la Magereza, Salum Msabaha, alisema asilimia 46 ya wafungwa na watuhumiwa waliopo mahabusu ni wa makosa ya udhalilishaji katika magereza ya Zanzibar.

Alisema awali asilimia 60 ya wafungwa huwa wanarejea makosa baada ya kumaliza vifungo vyao na kwa kuliona hilo magereza imeanzisha programu ya kuwafunza tabia njema wafungwa.



Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui (kushoto), akizungumza na timu ya Vodacom Tanzania inayoshughulikia mfumo wa kitaifa wa kuhudumia kinamama wajawazito na watoto wachanga pindi wanapopatwa na dharura (m-mama) ambao unategemewa kuzinduliwa visiwani humo hivi karibuni, ilipotembelea ofisini kwake mjini Unguja jana. Kampuni hiyo ilibuni mfumo huo ambao umekuwa suluhisho katika kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Dk. Mwinyi azitaka jumuiya za CCM kujijenga kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amezitaka jumuiya za chama hicho kujijenga kwa nguvu za kiuchumi ili zitekeleze majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

Alitoa rai hiyo Ikulu, Zanzibar wakati alipofanya mazungumzo na uongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT Taifa).

Alisema lazima jumuiya ziwe na nguvu za kiuchumi ili zitekeleze kazi zao kwa wakati na kuongeza kuwa jumuiya isiyo na nguvu za kiuchumi ni ngumu kufanikisha malengo yake.

Dk. Mwinyi aliwataka kinamama hao kujiimarisha kiuchumi pamoja na kuwa na zana za kiuchumi vikiwamo vitendea kazi imara.

Aidha, aliwaahidi kufanyakazi nao kwa karibu katika kufanikisha malengo ya jumuiya hiyo.

Hivyo aliwataka viongozi hao kuitumia mikutano ya hadhara kuwaeleza wanachama wao mafanikio yaliyofikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa ilani ya chama.

"Suala la kuitumia mikutano ya hadhara kuelezea mafanikio ya ilani ya chama ni jambo la msingi, wenzetu wakifanya mikutano watazungumzia kasoro, lakini nyinyi itumieni mikutano kuzungumzia mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi chote," alisema.

Aliwataka viongozi hao kupata mafunzo ya mara kwa mara kwa lengo la kutekeleza kazi zao kwa ufanisi kwa mujibu wa taratibu za jumuiya yao. Kuhusu kuwawezesha kiuchumi, Dk. Mwinyi aliiahidi kushirikiana nao katika kuzifikia fursa za kiuchumi ili kuziwezesha jumuiya nyingine ziwe na nguvu za kiuchumi.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko tayari kufanya kazi na asasi nyingine zikiwamo asasi zisizo za serikali na taasisi za vyama vya siasa ili kutimiza yote yanayowagusa wananchi.

Akizungumzia masuala ya mikopo kwa wanawake na watu wenye ulemavu, Dk. Mwinyi, alisema serikali imejipanga kuhakikisha inawafikia walengwa wengi kwa kupunguza msururu wa usumbufu kwenye upatikanaji wa fedha hizo ambazo hutolewa na halmashauri.

Mwenyekiti wa UWT Taifa, Marry Chatanda, ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Halmashauri ya Taifa, alisema miongoni mwa matarajio ya jumuiya hiyo ni kuimarisha uhai wake na kuongeza wanachama.

Pia alisema matarajio mengine ni kufanya ziara, kuandaa mikutano ya hadhara kwa kuelezea utekelezaji wa ilani ya chama.

Aidha, alieleza mikakati ya jumuiya hiyo kwa kuwatumia Watanzania waishio ughaibuni katika kusukuma mbele maendeleo ya wanawake nchini.

Alisema UWT inatarajiwa kuwa mtandao wa wanawake wenye nguvu zaidi wenye uchechemuzi ndani na nje ya nchi.

# Jeshi la Polisi lakamata madumu 2,000 ya mafuta ya kula

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MADUMU 2,000 ya mafuta ya kula yamekamatwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja ambayo yaliibiwa katika ghala moja la mfanyabiashara visiwani humo.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, ACP Abubakar Khamis Ali, alisema jeshi hilo lilifanikiwa kukamata mafuta hayo eneo la Marumbi Mkoa wa Kusini Unguja yakiwa ndani ya ghala linalomilikiwa na Muharami Khamis Saliboko (22) mkazi wa Chwaka.

Alisema tukio hilo lilitokea Januari 7, mwaka huu, majira ya saa 4:00 usiku eneo la Mombasa Unguja, kwamba wezi kwa kushirikiana na mlinzi wa ghala, Amos Laizer Molel walivunja na kuiba madumu 2,000 ya mafuta ya kula yenye ujazo wa lita 20 mali ya Kampuni ya Al-Azizia yote yakiwa na thamani ya Sh. milioni 160.

Alisema katika msako huo jeshi hilo pia lilifanikiwa kukamata magari manne yenye namba Z.951 AU aina ya fuso ikiendeshwa na Juma Ali Othman, miaka (29) mkazi wa Kibandamaiti na gari Z.943 JJ aina ya fuso iliyokuwa ikiendeshwa na Rajabu Kombo Makame, miaka (30) mkazi wa Shaurimoyo.

Alitaja gari nyingine ni Z.598 CW aina ya canter iliyokuwa ikiendeshwa na Mohammed Ali Mwadini miaka (30) mkazi wa Chumbuni na Z.850 FM aina ya fuso iliyokuwa ikiendeshwa na Hamad Shaaban Salum miaka (47) mkazi wa Mwera ambapo kila gari moja ilipakia mafuta dumu 500 kati ya madumu 3,000 yaliyokuwamo katika ghala hilo.

Alisema magari hayo yalitumika kubeba madumu hayo kutoka Mombasa Wilaya ya Magharibi B" Unguja na kupeleka Mkoa wa Kusini Unguja.

Kamanda Abubakar alisema Jeshi la Polisi linawashikilia madereva hao na gari zao katika Kituo cha Polisi Mazizini huku juhudi za kuwakamata watuhumiwa waliokimbia zinaendelea.

Alisema Jeshi la Polisi pia linamshikilia Zakia Ali Machano (33) mkazi wa Manzese Dar es Salaam kwa kosa la kuiba pesa kwa njia ya mtandao.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Januari 13, mwaka huu, majira ya saa 10:30 jioni Mtaa wa Kwamchina visiwani humo baada ya kutuma ujumbe hewa katika simu ya wakala wahuduma za kifedha ukionesha kuwa ametoa Sh. milioni moja na wakala alimpatia mtuhumiwa huyo kiasi hicho.

Alibainisha kuwa baada ya muda mfupi wakala alibaini kwamba hakuna muamala uliofanyika ndipo alitoa taarifa polisi na kufanikisha kumkamata mtuhumiwa huyo.

Alisema baada ya mahojiano mtuhumiwa huyo alikiri kushiriki matukio mbalimbali ya wizi kwa njia ya mtandao akishirikiana na wenzake ambao bado wanatafutwa.

Kaimu kamanda huyo alisema katika tukio lingine lililotokea Januari 13, mwaka huu majira ya 12:30 jioni huko Magogoni, Jeshi la Polisi lilimkamata Juma Ahmada Juma (42) mkazi wa Mwera kwa kosa kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Alisema mtuhumiwa huyo alijipatia Sh. milioni 3.95 kutoka kwa watu watano maeneo tofauti baada ya kuwadanganya kuwa atawapatia ajira katika Idara ya Usalama wa Taifa.

Aidha, alisema mtuhumiwa huyo anashikiliwa na Jeshi la Polisi na upelelezi utakapokamilika atafikishwa mahakamani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**ILIYOPO DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA RUFAA YA MADAI NA. 247 LA 2017**
**EMMANUEL BILINGE……………………MRUFANI**
**DHIDI YA**
**JOSEPH JOHN PEMBE………………MRUFANIWA**

**KWA: JOSEPH JOHN PEMBE – POPOTE ULIPO**

Unajulishwa kwamba shauri la Rufaa ya Madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa tarehe 6/2/2023 saa tatu kamili asubuhi (3:00) katika Mahakama ya Rufani Tanzania ikiketi Dar es salaam. Unatakiwa kufika bila kukosa mwenyewe au mwakilishi wako anayetambulika kisheria. Pia usipofika mwenyewe au mwakilishi wako, shauri hili litasikilizwa bila ya uwepo wako.

Imetolewa leo hii tarehe 06 Mwezi Januari, 2023.

THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA

R. W. Chaungu
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI(T)

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

ELISAMEHE MBWAMBO NGODA anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba: MC474 ADN, CHASSIS NAMBA: KE7KEFPK009874 na ENGINE NAMBA: 162FMJD5080577. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/23347/2023

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Josephat Shangazi Samson anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya **SANLG** yenye namba **MC 123 BPM** yenye jina la Kampuni Wu Zhou Investment Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Josephat Shangazi Samson kwa simu namba **0625998420.**

Taarifa ya Polisi **SHI/SHI/RB/5754/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

OBEY ASSERY NKYA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA LAND CRUISER yenye usajili namba: T494 DGL , CHASSIS NAMBA: JTEHC05J00439090 na ENGINE NAMBA:1HD0305110. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: DAR/BUG/RB/22949/2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 2476/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SHINUNA WA SULTANI HEMED**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SAMIR SALIM OMAR**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 14 Mwezi wa 02 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia; Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 16 Mwezi wa 01 Mwaka 2023.

MARCAS
DEBT COLLECTORS AND AUCTIONEERS (T) LTD.

**TENDER FOR SALE OF PLOT NO.66 BAHARI BEACH AREA KINONDONI MUNICIPALITY IN DAR ES SALAAM CITY**

Pursuant to instructions given to us by our Principal BOA BANK of Head Office

| PLOT NO. | | DESCRIPTION OF PROPERTY | LOCATION |
|---|---|---|---|
| 66 | ZACHARIA HANS POPPE | CT NO. 41673 PLOT NO. 66 BAHARI BEACH AREA, KINONDONI MUNICIPALITY IN DAR ES SALAAM CITY | KINONDONI MUNICIPALITY IN DAR ES SALAAM CITY |

**TERMS AND CONDITIONS OF TENDER:**

1. Interested tenders are advised to get further information of property for sale from the office of MARCAS DEBT COLLECTORS AND AUCTIONEERS (T) LTD. ARUSHA SAFARI HOTEL 2ND FLOOR RM NO: 316 & DAR ES SALAAM KITALU NO: 30E, KIWANJA NO: 09, MTA WA KABANGWA KATA YA MWANANYAMALA, MUNICIPAL YA KINONDONI
2. Inspection and search reports of the property are to be conducted by interested before submission of the bids for purchase of the property.
3. Deadline for submission of the bid documents shall be on Thursday 12th January, 2023 - Thursday 26th January
4. Tenders shall be opened at office MARCAS DEBT COLLECTORS AND AUCTIONEERS (T) LTD.
5. Telegraph, faxes, electronically mailed and late submission of bid documents shall not be accepted.
6. Bid Documents should be in plain envelope with outer cover clearly marked "TENDER NO. MDC-BOA/2023/12 addressed and delivered to MARCAS DEBT COLLECTORS AND AUCTIONEERS (T) LTD. ARUSHA TANZANIA
7. The winner of the tender must be able to deposit 25% of the bid price 3 days being declared and notified the successful winner of the tender. He must be able to pay the remaining 75% within fourteen (14) days from the award letter.
8. If the successful winner fails to pay the remaining 75% of the bid amount within the specified fourteen days after the award letter, the deposited amount will be forfeited and the property resold by new tender after fresh notification.

**FOR MORE DETAILS CONTACT: ARUSHA 0787 151 550 DAR ES SALAAM 0783 721 729**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Milipuko yarindima kambi ya jeshi Somalia

**Mogadishu, SOMALIA**

MILIO ya risasi na milipuko mikali, imesikika katika kambi ya kijeshi katika ya mji wa Hawadley katika eneo la Shabelle ya kati nchini Somalia.

Mamlaka zinaamini kwamba, shambulizi hilo limetekelezwa na watu wanaoshukiwa kuwa wanachama wa kundi la wanajihadi la al-Shabab.

Ofisa mkuu wa jeshi, ni miongoni mwa waliouawa katika uvamizi huo, lakini bado hakuna taarifa kamili kuhusu waliouawa.

Tukio hilo, linakuja siku chache baada ya jeshi kuteka bandari ya kimkakati ya Haradhere, ambayo imekuwa ikishikiliwa na kundi la kijihadi kwa miaka 15.

Al-Shabab wamepoteza maeneo mengi tangu mwaka jana, wakati wanajeshi wa serikali wakisaidiwa na wanamgambo wa koo walipoanzisha mashambulizi kusini na katikati mwa Somalia.

Lakini kundi hilo, limeendelea kufanya mashambulizi dhidi ya majengo hasa ya serikali na wanajeshi wa Umoja wa Afrika. ***BBC***



Baadhi ya watu wakiwa kwenye kumbukumbu ya Martin Luther King Jr. Kumbukumbu iliyofanyika mbele ya sanamu yake katika kampasi ya Chuo Kikuu cha Texas, Austin, nchini Marekani juzi. **PICHA: XINHUA**

# IS yateka wanawake 50 mchana

**Ouagadougou, BURKINA FASO**

TAKRIBANI wanawake 50 wametekwa nchini Burkina Faso na wenye msimamo mkali wa Islamic State (IS), katika eneo la Sahel, kaskazini mwa Burkina Faso, wiki iliyopita kwa mujibu wa maofisa waliozungumza Jumatatu.

Utekaji huo, ulitokea Januari 12 na 13, mwaka huu takriban kilometa 15 kutoka Arbinda katika jimbo la Soum, alisema Luteni Kanali Rodolphe Sorgho, ambaye ni Gavana wa Sahel, katika taarifa yake.

Wanawake walitekwa walipokuwa nje wakichuma matunda.

Ghasia za kijihadi zinazohusishwa na kundi la Al Qaeda na IS zimegubika Burkina Faso na kusababisha mauaji ya maelfu ya watu na kukosesha makazi watu milioni mbili katika taifa hilo la Afrika Magharibi.

Kushindwa kwa serikali kuzuia mapigano kumesababisha hali kutokuwa na utulivu na kusababisha mapinduzi mawili ya kijeshi mwaka 2022.

***VOA***

# Tshisekedi amfurusha mshauri wake

**Kinshasa, DRC**

RAIS Félix Tshisekedi, amemwondoa mshauri wake binafsi baada ya kufanya mabadiliko katika ofisi yake.

Fortunat Biselele, mshauri wake wa kibinafsi aliyekuwa na ushawishi mkubwa katika Ikulu ya Kinshasa, amefutwa kazi, huku Serge Tshibangu, akithibitishwa kuendelea kusimamia mchakato wa amani Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Baadhi ya wafanyakazi Ikulu ya Kinshasa, wametenguliwa huku wengine walioonekana kuwa nguzo ya utawala wake na waaminifu kwake na wenye kufanya kazi kwa ufanisi wakithibitishwa.

Fortunat Biselele, alikuwa anabeba mzigo mkubwa wa uhusiano kati ya Kigali na Kinshasa.

Alikuwa kiungo muhimu katika kuyaunganisha mataifa hayo mawili kiuchumi na kiusalama.

Lakini kitumbua kilianza kuingia mchanga wakati waasi wa M23 walipokuwa wakisonga mbele kwenye uwanja wa mapambano huko Kaskazini mwa Mkoa wa Kivu, hivyo ushawishi wake ukapungua hata baadhi katika ofisi ya rais wakaanza kumshuku na kabla ya kuachishwa kazi na alikuwa hahusishwi tena katika mikutano.

Kabla ya kuwekwa kando, Fortunat Biselele, alihojiwa mara kadhaa na idara ya ujasusi na hata nyumba yake ilipekuliwa kulingana na duru za usalama.

Serge Tshibangu, alithibitishwa kuwa mkuu wa ufuatiliaji wa michakato mikuu ya amani na ameteuliwa kuwa Mwakilishi Mkuu wa ufuatiliaji wa mkataba wa Luanda, pamoja na mchakato wa Nairobi.

Wakati huo huo, atalazimika kusimamia uhusiano wa kweli na M23, kupitia wajumbe kutoka Kigali na pia kusimamia mazungumzo na vikundi vingine vyenye silaha.

Wiki moja kabla ya kuachishwa kazi, alisikika akieleza kupitia mahojiano kwamba, Rais Tshisekedi alivyotumwa Kigali kwa Rais Kagame, kuzungumzia masuala ya madini ili kila upande unufaike, inaweza kuwa sababu ya kutenguliwa kwake.

***RFI***

# Upinzani Afrika Kusini kuishtaki serikali uhaba wa umeme

**Johannesburg, AFRIKA KUSINI**

MAKUNDI ya upinzani Afrika Kusini, Chama cha Wafanyakazi na wamiliki wa biashara wametishia kuishtaki serikali kutokana na kukatika kwa umeme nchini humo.

Wameipa serikali hadi Ijumaa, kuweka nishati ya umeme kutengamaa la sivyo wachukuliwe hatua za kisheria kwa kukiuka wajibu wake wa kutoa umeme.

Wameandika barua ya madai kwa Waziri wa Mashirika ya Umma, Pravin Gordhan na Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Shirika la Serikali ya Eskom, Andre de Ruyter, wakisema kuwa serikali inakiuka wajibu wake wa kutoa umeme. Kukatika kwa umeme kumeendelea kwa zaidi ya muongo mmoja, huku kukiwa na usimamizi mbovu na ufisadi katika kampuni ya serikali ya Eskom.

Hivi karibuni, nchi imekuwa ikikosa umeme hadi saa 10 kila siku. Tatizo hilo limemfanya rais kughairi safari ya kwenda kwenye Kongamano la Kiuchumi la Dunia huko Davos, ili kufanya mikutano nchini kwake na viongozi wa biashara na wafanyakazi.

***BBC***

# SIMBA QUEENS, YANGA PRINCESS VITANI LEO

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za Simba Queens na Yanga Princess, leo zitakuwa kwenye viwanja tofauti ugenini kusaka pointi tatu kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu ya soka Wanawake.

Simba ambayo wamemrejesha winga wao hatari aliyekuwa akicheza soka la kulipwa nchini Morocco, Mwanahamisi Omari na kumsajili Asha Rashid Mwalala itakuwa kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyangao kucheza dhidi ya Amani Queens.

Yanga Princess ipo mkoani Iringa na leo itashuka Uwanja wa Chuo cha Mkwawa kucheza dhidi ya Ceasiaa Queens, huku vinara wa ligi hiyo, JKT Queens itakuwa kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam kuwakaribisha The Tigers Queens kutoka Arusha na Alliance Girls itakuwa nyumbani, Uwanja wa Nyamagana, Mwanza ikiwa mwenyeji wa Mkwawa Queens.

Fountain Gate Princess itakuwa kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma kucheza dhidi ya Baobab Queens.

Hii ni raundi ya sita ya ligi hiyo ambayo inaongozwa na JKT Queens yenye pointi 13, huku Fountain Gate Princess ikiwa kwenye nafasi ya pili na pointi 12 na nafasi ya tatu inachukuliwa na Yanga Princess yenye pointi 10.

Simba Queens ipo kwenye nafasi ya nne ikiwa na pointi 10, lakini ikiwa na mabao 10 ya kufunga ikizidiwa mabao mawili na Yanga Princess.

Alliance Girls ipo kwenye nafasi ya tano na pointi zake saba, Ceasiaa ina pointi sita, Baobab Queens na Amani Queens zina pointi nne kila moja na The Tigers Queens na Mkwawa zina pointi moja kila moja.



Mchezaji wa Yanga, Fiston Mayele (katikati), akichuana na wachezaji wa Ihefu wakati wa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baina ya timu hizo uliopigwa juzi jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA:YANGA**

# Azam wametufunga kwa ubora wao - Kocha Prisons

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Prisons, Patrick Odhiambo, amesema kipigo cha mabao 3-0 walichokipata kutoka kwa Azam FC kimetokana na ubora wa wapinzani wao na si vinginevyo.

Akizungumza juzi usiku baada ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye Uwanja wa Azam Complex, kocha huyo alisema kimbinu wao walikuwa bora, lakini mechi hiyo iliamuliwa na kiwango na uwezo wa mchezaji mmoja mmoja ambapo wao wanazidiwa na wale wa Azam.

"Mechi tumepoteza kwa sababu ya ubora wa wachezaji mmoja mmoja, ukiangalia wenzetu wana wachezaji bora ndicho kilichotuangusha," alisema.

"Ila kusema kweli si vizuri sana nzuri kupoteza tena kwa mabao mengi kama tunavyofanya, mabeki wangu wanaonekana kuwapata nafasi sana washambuliaji wa timu pinzani ya kuangalia lango, nitaenda kubadilisha hilo, lakini mashabiki wasiwe na wasiwasi hatuwezi kushuka daraja," alisema Odhiambo.

Hii ni mara ya pili mfululizo kwa Prisons kupoteza mechi kwa mabao mengi jijini Dar es Salaam, kwani Desemba 30, mwaka jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ilichapwa mabao 7-1 dhidi ya Simba.

Naye Kocha Msaidizi wa Azam FC, Aggrey Morris, aliwasifu wachezaji wake kwa kupambana na kujituma mpaka kufanikiwa kupata ushindi huo.

"Siyo kama Prisons walicheza vibaya, ila wachezaji wangu walipambana na kujituma zaidi ndiyo maana tumepata ushindi huu, tunamshukuru Mungu," alisema Aggrey.

Yalikuwa ni mabao ya Abdul Suleiman 'Sopu' dakika ya 48 na Kipre Junior dakika ya 70, wakati Yona Amos akiwa amejifunga dakika ya pili tu ya mchezo.

Matokeo hayo yanaifanya Azam FC kufikisha pointi 44, moja nyuma ya Simba ambayo leo inacheza dhidi ya Mbeya City, ikiendelea kusaliwa kwenye nafasi tatu, wakati Prisons ikiwa kwenye nafasi ya 11 kwa pointi 21, zote zikicheza mechi 20.

# JKU SC yaipania Uhamiaji leo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya JKU SC imesema inahitaji kushinda mchezo wao wa leo Jumatano dhidi ya Uhamiaji ili isogee katika nafasi nne za juu za Ligi Kuu ya Zanzibar inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

JKU ipo nafasi ya tano ikiwa na alama 24 wakati wapinzani wao Uhamiaji wakiwa nafasi ya nane na alama zao 23 timu zote zikiwa zimecheza michezo 15.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa timu hiyo, Shehe Mohamed Khamis, amesema anajua anaenda kucheza na timu ngumu ambayo amepishana nayo alama moja hivyo utaufanya mchezo huo kuwa mgumu zaidi kila timu ikiitaji alama tatu.

Alisema kuelekea mchezo huo amepanga kuwashusha dimbani wachezaji ambao anaamini wakicheza vizuri na kufata maelekezo ya mwalimu watafanikiwa kupata alama tatu.

Alisema mpaka sasa wachezaji wote ambao wanatarajiwa kuwa sehemu ya kikosi hicho wapo vizuri kiafya na hakuna mchezaji majeruhi.

"Tunashuka uwanjani kwa kusaka alama tatu muhimu ili tusonge mbele katika msimamo wa Ligi, kama tunavyojua kwa mzunguko huu kila timu imejiimarisha katika dirisha dogo hivyo lazima tucheze kwa umakini mkubwa ili tufanikiwe," alisema.

Aidha katika mchezo wa ligi hiyo hapo juzi, Zimamoto SC ililazimishwa sare ya 1-1 na Kipanga FC mchezo uliochezwa katika dimba la Amaan wakati huko uwanja wa Finya Kisiwani Pemba Wenyeji Jamhuri wamefanikiwa kupata alama tatu baada ya kuifunga Taifa Jang'ombe bao 1-0.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RICE ATAKIWA ARSENAL

KLABU ya Arsenal imememfanya Declan Rice kuwa mlengwa wao mkuu wa uhamisho wa majira ya joto na wana imani kuwa wanaweza kushinda Chelsea ili kumsajili kiungo huyo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 24. ***(Times)***

### BELLINGHAM NA MAZUNGUMZO

MKURUGENZI wa michezo wa Borussia Dortmund, Sebastian Kehl, anapanga mazungumzo na kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham na wazazi wake kuhusu mustakabali wa kinda huyo mwenye umri wa miaka 19 na amesema hakujawa na ofa yoyote kwa ajili yake. ***(Kicker)***

### RAPHINHA HAONDOKI

WINGA wa Brazil, Raphinha amekuwa akihusishwa na Arsenal, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 hana nia ya kuondoka Barcelona Januari hii. ***(Mundo Deportivo)***

### GALLAGHER ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inatazamia kuwasajili kiungo wa kati wa Chelsea, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 22, pamoja na winga wa Morocco mwenye umri wa miaka 29, Hakim Ziyech mwezi huu. ***(Telegraph)***

### EBERL KUTUA CHELSEA

MKURUGENZI wa michezo wa RB Leipzig, Max Eberl amesema "dalili ziko wazi" kwamba fowadi wa Ufaransa, Christopher Nkunku mwenye yumri wa miaka 25 atajiunga na Chelsea. ***(Bild)***

### GONZALEZ ANYATIWA

KLABU ya Newcastle imejiunga na Leicester City katika mbio za kumnunua fowadi wa Fiorentina na Argentina, Nico Gonzalez, lakini klabu hiyo ya Serie A haitamruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kwenda kwa chini ya pauni milioni 40. ***(TuttoMercatoWeb)***

### HINCAPIE ATAKIWA

KLABU ya Everton na Newcastle United inafanya mazungumzo juu ya kumsajili mlinzi wa Bayer Leverkusen mwenye umri wa miaka 21, Piero Hincapie ambaye amekuwa akihusishwa na Tottenham Hotspur. ***(Football Insider)***

### OUNAHI AWANIWA LEEDS

KLABU ya Leeds United imeongeza dau lao la pauni milioni 22.2 kumnunua kiungo wa kati wa Angers, Azzedine Ounahi mwenye umri wa miaka 22. ***(90Minutes)***

### GORDON HATAKIWI

CHELSEA na Tottenham Hotspur hawana mpango tena na mshambuliaji wa Everton, Anthony Gordon mwenye umri wa miaka 21. ***(CaughtOffside)***

### CASTELLANOS AWINDWA

KLABU ya Brighton inavutiwa na mshambuliaji wa Argentina mwenye umri wa miaka 24, Valentin Castellanos, ambaye yuko kwa mkopo Girona kutoka New York City. ***(Independent)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# WAKILI AKATAA DEPAY KUJIUNGA INTER

●●●Asema jambo hilo kwa sasa haliwezekani na hakuna mazungumzo ya...

**BARCELONA, Hispania**

MEMPHIS Depay hatajiunga na Inter Milan kutoka Barcelona katika dirisha la Januari, wakili wake amesema.

Mshambuliaji huyo wa Uholanzi anatarajiwa kuondoka Barca mwezi huu, huku Inter ikiwa ni miongoni mwa klabu zinazoripotiwa kutaka kumsajili.

Baada ya Barcelona kumsajili Robert Lewandowski, Depay ame- [illegible] namba kwenye kikosi cha kwanza na ameanza mara mbili pekee kwenye mechi za Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, msimu huu.

Wakili wa Depay, Sebastian Ledure amekanusha madai kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ambaye anahusishwa na klabu ya Atletico Madrid, anaweza kuwa njiani kuelekea kule kwenye dimba la San Siro.

"Hakuna mazungumzo yanayoendelea kwa Memphis kujiunga [illegible] wambia mwandishi wa habari za usajili, Fabrizio Romano.

"Naweza kukataa kuhusu hilo, hakuna uwezekano kwamba tunajadili kuhusu hilo."

Fowadi huyo wa zamani wa Lyon na Manchester United alijiunga na Barca mwaka 2021 na hakutumika kama mchezaji wa akiba katika ushindi wa 3-1 wa Supercopa de Espana dhidi ya Real Madrid, Jumapili.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,067,6

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 18,19 NA 20 JANUARI 2023
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/01/23 | 18:00 | Talaea El Gaish vs Ismaily SC | 2.83 | 2.68 | 2.88 |
| 02. 18/01/23 | 19:00 | DR Congo vs Ivory Coast | 3.44 | 3.04 | 2.22 |
| 03. 18/01/23 | 22:00 | AC Milan vs Inter | 2.85 | 3.34 | 2.44 |
| 04. 18/01/23 | 22:45 | Livingston vs Dundee Utd | 2.43 | 3.23 | 2.83 |
| 05. 19/01/23 | 17:30 | Gaziantep BB vs Konyaspor | 2.53 | 3.22 | 2.53 |
| 06. 19/01/23 | 18:00 | National Bank vs El Ittihad Alexandria | 2.31 | 2.84 | 3.44 |
| 07. 19/01/23 | 23:00 | Villarreal vs Real Madrid | 3.03 | 3.43 | 2.21 |
| 08. 20/01/23 | 14:00 | Gokulam Kerala FC vs Real Kashmir | 2.25 | 2.98 | 3.12 |
| 09. 20/01/23 | 19:00 | Istra vs Slaven Belupo | 2.31 | 3.10 | 2.91 |
| 10. 20/01/23 | 20:30 | Sochaux vs Caen | 2.33 | 3.12 | 3.02 |
| 11. 20/01/23 | 21:30 | Cholet vs FC Martigues | 2.87 | 3.16 | 2.38 |
| 12. 20/01/23 | 21:30 | Saint Brieuc vs Paris 13 Atletico | 2.62 | 3.11 | 2.62 |
| 13. 20/01/23 | 21:30 | Villefranche Sur Saone vs Red Star | 2.66 | 3.21 | 2.52 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa, vodacom m-pesa, halopesa, airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# RICHARLISON AELEZEA MACHUNGU YA KOMBE LA DUNIA

**BARCELONA, Hispania**

RICHARLISON amesema kushindwa kwa Brazil katika robo fainali ya Kombe la Dunia dhidi ya Croatia ni "mbaya zaidi kuliko kumpoteza mwanafamilia".

Brazil ambao walikuwa wakipewa nafasi kubwa kabla ya michuano hiyo walishinda Kundi G na kuwalaza Korea Kusini 4-1 katika hatua ya 16 bora na kuongeza matumaini kwamba wanaweza kutawazwa ubingwa kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2002.

Lakini kampeni yao ilisimama katika hatua ya robo fainali nchini Qatar na kupoteza kwa mikwaju ya penalti kutoka kwa Croatia baada ya Marquinhos na Rodrygo kushindwa kufunga mikwaju yao ya penalti.

Kipigo hicho kilizua hisia kali kutoka kwa wachezaji kadhaa huku Neymar, ambaye aliipatia Brazil bao la kuongoza kwa muda wa ziada kabla ya Bruno Petkovic kufunga bao la kusawazisha.

Richarlison ameiambia ESPN: "Ilikuwa pigo, sijui. Nadhani ni mbaya zaidi kuliko kupoteza mwanafamilia.

"Ilikuwa ngumu kupona, hadi leo nikitazama video kwenye mitandao yangu ya kijamii inanihuzunisha.

"Lakini lazima tusonge mbele, mimi bado mdogo, nafikiri bado ninaweza kucheza Kombe la Dunia moja au mara mbili, nitaendelea kujifua kwa bidii ili mambo yaanze kusonga mbele."

Licha ya kumalizika kwa mchuano hiyo kwa kusikitisha, ilikuwa Kombe la Dunia la kwanza kwa Richarlison, ambaye alikuwa mfungaji bora wa Brazil akiwa na mabao matatu.

# Klopp hana mpango wa kujiuzulu

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema hataondoka katika klabu hiyo labda alazimishwe na amedokeza kuhitaji mabadiliko hapo kwenye dimba la Anfield wakati wa majira ya joto.

Matamshi ya Mjerumani huyo yanakuja huku kukiwa na mwenendo mbaya wa Wekundu hao, ambao wako katika nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England.

"Aidha, nafasi ya kocha inabadilika au mambo mengi yanabadilika," alisema Klopp.

"Labda kuna mahali tunapaswa kubadilisha mambo mengine. Tutaona hilo, lakini hilo ni jambo la siku zijazo. Kama majira ya joto au chochote. Sio sasa.

"Nina nafasi na muda wa kulifikiria. Tunapaswa kucheza soka bora zaidi sasa."

Liverpool walichapwa 3-0 na Brighton Jumamosi baada ya kile Klopp alichoeleza kuwa uchezaji "mbaya sana" na akasema timu yake ilibidi "kurejea kwenye misingi" ili kuboresha kiwango chao.

"Sikuwa katika hali kama hiyo mara nyingi, lakini najua jinsi inavyofanya kazi wakati mambo hayaendi vizuri," alisema.



15,605/-

# SABABU YA MWAMBUSI KUONDOKA IHEFU FC

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Ihefu, Juma Mwambusi ambaye hajaonekana kwenye timu hiyo tangu Januari 3 ilipocheza dhidi ya KMC na kushinda bao 1-0, amesema amejiweka kando kwenye kikosi hicho kwa ajili ya kushughulikia kwanza matatizo yaliyojitokeza ya kifamilia.

Mwambusi ambaye aliichukua Ihefu ikiwa kwenye hali mbaya na kuifanya kuwa timu tishio, ikiwa ndiyo timu pekee mpaka sasa iliyoifunga Yanga kwenye Ligi Kuu licha ya juzi kuchapwa bao 1-0 wakati yeye akiwa kando, amesema kuwa amejiweka kando kwanza ili ashughulikie matatizo hayo ya kifamilia na yakimalizika ndiyo atakuwa na neno la kuongea.

"Nimepumzika kidogo, nina majukumu mengine zaidi ya kuifundisha timu ya Ihefu, kwa muda huu sipo kwenye timu, kwa sasa ipo chini ya Zuberi Katwila ambaye yeye nimemkuta pale, nadhani kwa sasa wanaendelea vizuri kwenye mambo yao ya usajili kwa sababu mipango hiyo ilikuwa inaendelea.

Kuna mambo mengine yameingia kati hapa kwa hiyo nimeona kwanza niyashughulikie, akili yangu kwanza iwe kwenye hili jambo la kifamilia kwanza, nadhani baada ya kuweka sawa sawa nitakuwa na neno la kuzungumza kwa muda huu kwa kweli hakuna nitakachoelezea," alisema Mwambusi.

Alikiri kuwa ni kweli hakuwepo kwenye kikosi tangu Januari 3 ambapo ilicheza mechi ya Ligi Kuu dhidi ya KMC na kushinda bao 1-0, huku akiongeza kuwa hana tatizo lolote lililomfanya aondoke na pia hakuna anachowadai.

"Mimi na Ihefu hakuna tatizo lolote, ndiyo maana hata wao wameruhusu nikashugulikie hayo matatizo kwa sababu wameona ni ya umuhimu vile vile, na hakuna ninachowadai," aliongeza kocha huyo aliyetua kwenye klabu hiyo Septemba mwaka jana.



Wachezaji wa mpira wa kikapu wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA KAZI MOJA TU

INATOKA UK. 24

kupata matokeo mazuri na kujiweka katika nafasi nzuri katika msimamo wa ligi," alisema Anthony.

Alisema hawataki kuona kile kilichowatokea ndugu zao Prisons kwa kula kichapo cha mabao 7, jambo ambalo hawataki kuona yanatokea kwao kutofungwa kabisa au kupunguza idadi ya mabao.

# Nabi achimba mkwara

INATOKA UK. 24

kupoteza pointi ili kuchukuwa nafasi yao kupanda kileleni na wao kushuka chini.

"Ligi ya msimu huu ni ngumu kuliko msimu uliopita, tunahitaji kuwa makini kuhakikisha hatupotezi pointi maana tutawapa nafasi ya waliokuwa chini yetu kutumia fursa hiyo ya kuhakikisha wanatushusha na wao kutaka kupanda kileleni.

"Kuna ugumu unapotoka katika mapumziko na kuingia kwenye mechi hizi za mwanzo, pia maingizo mapya yanahitaji muda wa kujenga muunganiko pamoja na kuzoeana, kama ilivyo mechi ya leo kumpa nafasi Musonda (Kennedy).

"Mabadiliko ya wachezaji wengine kuondoka na kuingia, benchi la ufundi tutakiwa kutumia akili ya ziada kujenga kombinesheni ya wale wapya na waliokuwapo tangu awali katika kikosi," alisema Nabi.

Alisema hana mashaka na ingizo jipya la safu ya kiungo, Mudathiri Yahya kwa sababu ni mchezaji aliyemuhita tangu dirisha kubwa na sasa amefanikiwa kupata huduma yake.

"Mchezaji mzuri lakini yuko hapa anacheza na watu ambao aliwahi kucheza nao akiwa Azam FC, (Salum Abubakari) na Farid Mussa, hawezi kupata shida na nina imani hii ni asimilia 50 ya kiwango chake alichokionyesha leo (juzi)," alisema Nabi na kuahidi kuwa kiungo huyo atakuwa bora zaidi kila anapoendelea kuitumikia Yanga .

Kocha Mkuu wa Ihefu FC, Zuber Katwila, alisema vijana wake walipambana kwa kufuata alivyowaelekeza kiufundi katika uwanja wa mazoezi na kukipeleka katika mechi na kufanya vizuri zaidi.

Alisema licha ya kupoteza katika mchezo huo wachezaji walicheza vizuri na kipa wake alifanya kosa lililowafanya wapoteza mchezo huo.

"Siwezi kuhukumu kwa sababu mabeki walijitahidi kuokoa lakini bado Yanga walitumia nafasi," alisema.

"Kipa alifanya mazuri kuliko kosa ambalo amelifanya na kuruhusu bao na tunatarajia kufanyia kazi katika mazoezi na mechi ijayo tutaingia na mipango mingine."


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 21/01/23 | 18:00 | AFC Bournemouth vs Nottingham Forest | 2.60 | 3.20 | 2.65 |
| 02. 21/01/23 | 18:00 | Southampton FC vs Aston Villa | 2.80 | 3.30 | 2.42 |
| 03. 21/01/23 | 18:00 | Birmingham City vs Preston North End | 2.38 | 3.10 | 3.10 |
| 04. 21/01/23 | 18:00 | Blackpool vs Huddersfield Town | 2.27 | 3.15 | 3.20 |
| 05. 21/01/23 | 18:00 | Cardiff City vs Millwall FC | 2.95 | 3.05 | 2.48 |
| 06. 21/01/23 | 18:00 | Queens Park Rangers vs Swansea City | 2.55 | 3.25 | 2.70 |
| 07. 21/01/23 | 18:00 | Wigan Athletic vs Luton Town | 2.75 | 3.15 | 2.55 |
| 08. 21/01/23 | 18:15 | Espanyol Barcelona vs Real Betis Seville | 2.80 | 3.15 | 2.55 |
| 09. 21/01/23 | 22:00 | SC Cambuur vs Sparta Rotterdam | 2.95 | 3.35 | 2.31 |
| 10. 21/01/23 | 23:00 | RKC Waalwijk vs Go Ahead Eagles | 2.36 | 3.45 | 2.80 |
| 11. 22/01/23 | 13:30 | Gaziantep FK vs Sivasspor | 2.50 | 3.30 | 2.75 |
| 12. 22/01/23 | 15:00 | Sunderland AFC vs Middlesbrough FC | 2.80 | 3.25 | 2.45 |
| 13. 22/01/23 | 16:30 | Feyenoord Rotterdam vs Ajax Amsterdam | 2.85 | 3.55 | 2.28 |
| 14. 22/01/23 | 17:00 | Leeds United vs Brentford FC | 2.39 | 3.45 | 2.75 |
| 15. 22/01/23 | 17:00 | AC Monza vs Sassuolo Calcio | 2.26 | 3.30 | 3.10 |
| 16. 22/01/23 | 18:30 | Maritimo Madeira vs Estoril Praia | 2.55 | 3.15 | 2.80 |
| 17. 22/01/23 | 19:30 | Borussia Monchengladbac vs Bayer Leverkusen | 2.70 | 3.80 | 2.31 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 18/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1083 | Kariobangi Sharks vs Vihiga Bullets FC | 1.50 | 4.04 | 5.38 |
| 13:30 | 2310 | Khosheh Talaei vs Shams Azar Qazvin | 4.34 | 2.79 | 1.95 |
| 13:30 | 2950 | Fajr Sepasi vs Vanpars | 2.33 | 2.51 | 3.68 |
| 13:30 | 3038 | Pars Jonoubi Jam vs Kheybar Khorramabad FC | 2.95 | 2.29 | 2.75 |
| 13:30 | 3181 | Shahrdari Astara vs Mes Shahr-e Babak | 2.63 | 2.46 | 3.20 |
| 13:30 | 3413 | Arman Gohar Sirjan vs Chador Malu Yazd | 2.05 | 2.50 | 3.95 |
| 14:00 | 3833 | Neroca FC vs Tiddim Road Athletic Club | 2.70 | 3.17 | 2.42 |
| 14:30 | 1038 | Persita Tangerang vs Persebaya Surabaya | 2.84 | 3.20 | 2.29 |
| 14:30 | 3166 | Fatih Karagumruk vs Basaksehir | 3.16 | 3.42 | 2.03 |
| 15:00 | 5319 | Apollon Paralimniou vs Lamia | 8.05 | 4.34 | 1.34 |
| 15:10 | 1880 | AL Sahel SC vs Jeddah Club | 2.47 | 2.80 | 2.96 |
| 15:30 | 5305 | Al Faisaly (KSA) vs Alshoulla | 1.43 | 3.94 | 6.84 |
| 15:45 | 1168 | Haras EL Hodood vs El Daklyeh | 2.59 | 2.74 | 3.09 |
| 16:00 | 1781 | Club A Bizertin vs CS Chebba | 2.03 | 2.70 | 3.60 |
| 16:30 | 1591 | Venda Football Academy vs Uthongathi | 2.48 | 2.74 | 3.00 |
| 16:30 | 3454 | Polokwane City vs Platinum City Rovers | 1.78 | 3.01 | 4.88 |
| 16:30 | 5146 | Hungry Lion vs Mm Platinum FC | 1.90 | 2.95 | 4.24 |
| 17:00 | 2402 | Jamshedpur vs Bengaluru FC | 2.63 | 3.10 | 2.52 |
| 17:00 | 4160 | HNK Gorica vs Vsnk Varazdin | 2.31 | 3.22 | 2.81 |
| 17:45 | 2615 | Ankaragucu vs Besiktas | 2.73 | 3.40 | 2.27 |
| 18:00 | 1065 | Talaea El Gaish vs Ismaily SC | 2.54 | 2.84 | 3.04 |
| 18:00 | 2509 | FAR Rabat vs MAS Maghrib A Fes | 1.93 | 2.99 | 4.03 |
| 18:25 | 3352 | Najran SC vs AL Akhdood | 2.96 | 2.90 | 2.40 |
| 18:30 | 4944 | AEK Athens vs Panserraikos | 1.14 | 6.61 | 14.47 |
| 18:40 | 5424 | Al Ahli Jeddah vs AL Hazm | 2.21 | 3.01 | 3.17 |
| 19:00 | 1352 | Simba vs Mbeya City | 1.13 | 4.54 | 10.40 |
| 19:00 | 4185 | DR Congo vs Ivory Coast | 3.10 | 2.95 | 2.44 |
| 20:00 | 1721 | Enppi Club vs Coca Cola | 4.00 | 2.90 | 2.08 |
| 20:00 | 5626 | Olympiakos vs Aris Salonica | 1.53 | 3.74 | 5.61 |
| 20:15 | 5623 | Hassania Agadir vs CRS Salmi | 2.65 | 2.85 | 2.45 |
| 20:30 | 1692 | Oostende vs Royal Antwerp | 4.09 | 3.69 | 1.79 |
| 20:30 | 1709 | Umraniyespor vs Trabzonspor | 3.79 | 3.63 | 1.78 |
| 20:30 | 3238 | Cercle Brugge vs Union Saint Gilloise | 3.34 | 3.44 | 2.06 |
| 21:00 | 1689 | Sporting Gijon vs Valencia | 3.40 | 3.18 | 2.14 |
| 21:30 | 5147 | Bangu RJ vs Resende RJ | 2.23 | 2.90 | 3.26 |
| 21:30 | 5160 | PAOK vs Panathinaikos | 2.02 | 3.07 | 3.59 |
| 22:00 | 1389 | Athletic Bilbao vs Espanyol | 1.63 | 3.67 | 5.32 |
| 22:00 | 3179 | Senegal vs Uganda | 2.39 | 3.00 | 3.15 |
| 22:00 | 5504 | AC Milan vs Inter | 2.79 | 3.33 | 2.49 |
| 22:30 | 2772 | Difaa El Jadidi vs Ittihad Tanger | 1.38 | 4.24 | 7.25 |
| 22:45 | 1441 | Hearts vs Aberdeen | 2.15 | 3.43 | 3.14 |
| 22:45 | 2788 | Leeds vs Cardiff | 1.31 | 5.11 | 8.06 |
| 22:45 | 3910 | Celtic vs St Mirren | 1.11 | 8.38 | 18.96 |
| 22:45 | 4138 | Kortrijk vs RFC Seraing | 1.83 | 3.62 | 3.97 |
| 22:45 | 4314 | Livingston vs Dundee Utd | 2.43 | 3.23 | 2.83 |
| 22:45 | 5652 | Anderlecht vs Zulte Waregem | 1.53 | 4.39 | 5.19 |
| 23:00 | 1763 | Betis vs Osasuna | 2.09 | 3.18 | 3.55 |
| 23:00 | 2664 | Kilmarnock vs Rangers | 8.18 | 5.18 | 1.32 |
| 23:00 | 3356 | Crystal Palace vs Manchester Utd | 4.10 | 3.48 | 1.82 |
| 23:00 | 5470 | Levante vs Atletico Madrid | 4.56 | 3.44 | 1.77 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatano Januari 18, 2023
Nipashe



UKURASA 21

## Wakili akataa Depay kujiunga Inter

# SIMBA KAZI MOJA TU LEO

...Inaivaa Mbeya City katika mchezo wa kwanza wa Kocha Mkuu Oliveira kwenye Ligi...

**Na Saada Akida**

TIMU ya Simba leo inashuka kwenye dimba la Benjamin Mkapa kusaka pointi tatu muhimu dhidi ya Mbeya City katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kikosi cha Simba kilirejea nchini jana kikitokea Dubai ambako kiliweka kambi ya mazoezi ya siku 10 kwa ajili ya kujiandaa na michezo iliyoko mbele yao ya ligi hiyo na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Katika mchezo wa mzunguko wa kwanza Simba ililazimishwa sare ya kufungana bao 1-1 na Mbeya City katika Uwanja wa Sokoine, Mbeya.

Wakati Simba akili na nguvu zao ni kusaka pointi tatu muhimi, wao Mbeya City wataingia kwa heshima kubwa na tahadhari baada ya kushuhudia ndugu zao Prisons kukutana na kipigo cha mabao 7.

Kuelekea mchezo huo Kocha Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda, amesema wamejiandaa vizuri na kambi ya Dubai imemsaidia Kocha Roberto Oliveira kuandaa kikosi chake na wachezaji kupata mbinu na ufundi.

"Tunarejea nyumbani kujiandaa na michezo ijayo ikiwamo mechi yetu dhidi ya Mbeya City, tumejiandaa vizuri na tayari kwa mchezo huo kuhakikisha tunapata matokeo mazuri ili kufikia malengo yetu," alisema Mgunda.

Alisema mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu wanahitaji alama tatu na wapinzani wao wanahitaji kuleta ushindani mkubwa ili kupata matokeo mazuri.

Kwa upande wa Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema baada ya siku 10 za kambi na kumpa nafasi Kocha Mkuu Oliveira kuwafahamu wachezaji wake ana uhakika watatumia mbinu na falsafa zake za kiufundi ili kupata ushindi.

Alisema kikosi kipo vizuri na hakuna wachezaji majeruhi zaidi ya wawili, Mosses Phiri na Peter Banda ambao wako katika programu maalum ya kujiweka sawa.

"Tunarejea kambini moja kwa moja na tayari kwa ajili ya mchezo wetu dhidi ya Mbeya City, tutawakosa Phiri na Banda bado hajakuwa fiti kucheza mechi ya ushindani kutokana na hawajakuwa na utimamu wa mwili," alisema Ahmed.

Aliwataka mashabiki kujitokeza kwa wingi kwa sababu ni mechi ya kwanza ya Kocha Robertinho, lakini kuona kikosi chao baada ya kutoka kambini Dubai.

Naye Kocha Msaidizi wa Mbeya City, Antony Mwamlima, alisema wamefika salama Dar es Salaam na wako tayari kwa ajili ya mchezo dhidi ya Simba na watacheza kwa tahadhari kubwa.

"Hatukuwa na matokeo mazuri katika michezo mitatu ya nyuma, kwa mchezo wa kesho (leo) tunaangalia ni jinsi gani ya

INAENDELEA UK. 23



Wachezaji wa Simba, Clatous Chama (kushoto) na Shomari Kapombe wakijifua mazoezini. **PICHA: SIMBA**

## Nabi achimba mkwara Yanga

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, amepiga mkwara kwa kusema atamwadhibu mchezaji yeyote atakayeonesha utovu wa nidhamu bila kujali umuhimu wake katika kikosi cha kwanza cha timu hiyo.

Nabi amesema hayo baada ya kukamilika kwa dakika 90 za mchezo uliopigwa juzi wakati Yanga ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Ihefu FC kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kauli hiyo ya kocha huyo ni baada ya kuchukizwa na baadhi ya wachezaji ambao hawakufuata sheria za timu hiyo huku inadaiwa Mtendaji Mkuu wa Yanga, Andre Mtine, amepanga kumpa adhabu, Bernard Morrison kutokana na utovu wa nidhamu, ambaye hadi sasa hajaungana na kikosi cha timu hiyo ikidaiwa yuko kwao Ghana.

Nabi alisema mchezo wa mpira wa miguu ni muunganiko wa wachezaji wote na kila mmoja anatakiwa kuheshimu na kufuata sheria na kanuni za timu zilizowekwa.

"Mchezaji yeyote anayesajiliwa na kukabidhiwa kwenye benchi la ufundi ni mali ya kocha na anatakiwa kufuata sheria za timu, hatuogopi mtu ambaye hataheshimu sheria za timu. Hata mchezaji huyo ni muhimu katika timu, kipenzi cha mashabiki au viongozi akionyesha utovu wa nidhamu ataadhibiwa tu," alisema Nabi.

"Nimewaeleza viongozi juu ya huu msimamo wangu wa kutoa adhabu kwa watovu wa nidhamu hata kama huyo mchezaji muhimu au anatembea juu ya hewa lazima kuheshimu sheria za timu," aliongeza.

Kuhusu matokeo ya mchezo huo na Ihefu, kocha huyo alisema anawapongeza wachezaji wake kujitolea na kupambana kwa kuvuna alama tatu muhimu kwa kuwa mchezo ulikuwa wa ushindani mkubwa.

"Dakika 45 kipindi cha kwanza kilipokamilika niliwaeleza wachezaji wangu vyumbani kutulia zaidi ili kutafuta ushindi kwa sababu ya ubora wa wapinzani wetu," alisema.

Alisema mechi ilikuwa ya ushindani mkubwa kwani Ihefu walicheza kwa kiwango kizuri kwa sababu walikuwa tayari wamejiandaa kwa mchezo huu.

Kocha huyo alisema wanahitaji kuwa makini kila mechi kusaka pointi muhimu kwa sababu wanaowafuata katika msimamo watajua faida ya wao

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >